# Nipashe

Alhamisi Desemba 10, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580425

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US


ama AFYA NA MAZINGIRA



Halmashauri ya Tarime yaweka kituo afya cha kisasa, kilio chake wataalamu





Vita kukabili corona vimeshamiri, kufikia wengi ng'ambo ya Afrika, ni kitendawili

**Tafsiri mpya ya Msalaba Mwekundu itakavyohudumia afya miaka 5 ijayo**



UKURASA 11

**LORI** la mafuta lakamatwa na viroba 81 vya bangi

UKURASA 4



**DAKTARI** aieleza korti alivyompokea Mawazo akiwa hoi bin taabani

UKURASA 8

# Magufuli atoa maagizo mazito kwa mawaziri

**Ataka** kila mmoja kuwajibika, ataja sababu kuteua wazee, Ummy kwenda Makamu wa Rais...*Uk. 2 & 3*



Dk. Dorothy Gwajima
"Yale uliyokwamishwa sasa kaagize na yatekelezwe."





Geoffrey Mwambe
"Mapinduzi ya viwanda yakuze uchumi."

## Wafungwa 256 waliohukumiwa kunyongwa sasa kutumikia maisha

UKURASA 2



Dk. Medard Kalemani
"Kasi ya usambazaji umeme iongezeke."



Prof. Kitila Mkumbo
"Hakikisha ndani ya siku 14 wawekezaji wanapata vibali."



Ummy Mwalimu
"Tumekupeleka pale ukafanye mabadiliko, palikuwa panalegalega."



Prof. Adolph Mkenda
"Tunataka mabilionea wapatikane kupitia kilimo."




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## ...Anyang'anywa tonge mdomoni kwa kushindwa kusoma kiapo

UK. 3


**MICHEZO** FIFA KUIFUNGIA SIMBA KUSAJILI MIAKA 3 UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Wafungwa 256 waliohukumiwa kunyongwa sasa kutumikia maisha

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli jana, alitangaza kuwabadilishia adhabu wafungwa 256 waliohukumiwa kunyongwa, badala yake aliagiza wakatumikie kifungo cha maisha gerezani, sambamba na adhabu kali. Kadhalika, alitoa msamaha na kupunguziwa kifungo kwa wafungwa 3,316 waliohukumiwa kwa makosa madogo, waliotumikia kifungo gerezani kwa muda mrefu, pamoja na wale waliobakiza siku chache kumaliza adhabu zao.

Alitoa maagizo hayo jijini Dodoma wakati akiwaapisha mawaziri na manaibu mawaziri aliowateua hivi karibuni, hafla iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali na wastaafu.

Rais Magufuli alisema: "Leo ni sikukuu ya Uhuru wa taifa letu kutimiza miaka 59. Nataka kuwapongeza Watanzania wote kwa kusherehekea siku hii muhimu ya ukombozi wa taifa letu."

Aliongeza: "Najua katika kipindi cha miaka mitano ya utawala wangu mpaka leo nilitakiwa kunyonga watu 256, waliohukumiwa kunyongwa. Lakini sijanyonga hata mmoja."

Rais Magufuli alisema: "Na wale wafungwa 256 kwa mamlaka niliyopewa, nawapunguzia kifungo chao cha kunyongwa, sasa wafungwe maisha. Wapo walioua, wengine waliua mmoja, wawili, watatu. Mimi sheria inanitaka niue 256, nani mwenye dhambi zaidi? Huyo aliyeua mmoja au mimi niliyeua 256?"

Aliendelea: "Nimeshindwa kuwaua, nawaomba mnisamehe kwenye hilo, mimi nitakuwa muuaji wa kuuawa kwa sababu wenzangu waliua mmoja, wawili, watatu, wakahukumiwa kunyongwa, si nafuu na mimi nihukumiwe kunyongwa hapo hapo kuliko kupelekwa mahakamani. Kwa hiyo nimeshindwa."

Hivyo, Rais Magufuli aliagiza Wizara ya Mambo ya Ndani kushughulikia taratibu za wafungwa hao kubadilishiwa kifungo.

Rais Magufuli alisema: "Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kashughulikieni hili kwa mujibu wa sheria, wote wafungwe maisha na washiriki katika kufanya kazi."

"Pia wafungwa 3,316 wenye makosa madogo madogo, makosa ya kuiba kuku, wengine wametumikia kifungo chao muda mrefu na wamebakiza siku chache kumaliza kifungo, nimekubali wapunguziwe kifungo na wengine wasamehewe kwa mujibu wa sheria," alisema.

bgtl

**BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA(MARUDIO)**

Kwa Idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK** *Tunatoa* notisi ya siku kumi na nne(14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo wake kwa **MNADA WA HADHARA**.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO |
|---|---|---|
| 1. | A BETTER LIFE INVESTMENT/ PAYAS REUBEN MOREMI | Nyumba ya makazi yenye hati Na.51480 Plot Na 668/1 Na 690/1 Block E Gongo La Mboto Dar Es Salaam kwa jina la PAYAS REUBEN MOREMI |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Mawasiliano**

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road.
Green Acres Building, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
0715363537/0765363537

AU

Mkurugezi Mtendaji
Equity Bank (Tz) Limited
Head Office,
Ohio Street- Golden Jubilee Towers
P.O. Box110183
DAR ES SALAAM
email: equitybank@co.Ke

# JPM awapa maagizo mazito mawaziri

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli jana, aliwaapisha mawaziri na naibu mawaziri na kuwapa maagizo mazito katika utekelezaji wa majukumu yao.

Wakati akitoa maagizo hayo pia alieleza baadhi ya mambo ambayo mawaziri waliokuwa kwenye baraza lililopita pamoja na wapya walipokuwa katika nafasi mbalimbali walionyesha udhaifu katika utekelezaji wa kazi zao.

Akizungumza jana Ikulu Chamwino, Dodoma baada ya kuwaapisha, Rais Magufuli alisema uteuzi wao umezingatia mambo mengi yakiwamo nafasi katika mikoa ili kuweka uwiano.

Kutokana na kuwateua katika nafasi hizo, aliwataka wakatekeleze majukumu yao na kumtanguliza Mungu kwa sababu Watanzania wana matumaini makubwa juu yao.

"Kama ni matatizo ya maji, miradi ya maji ikakamilike. Watanzania wamechoka kusikia upembuzi yakinifu, mchoro sanifu, wanataka maji.

"Mkafanye uamuzi ni nafuu mfanye uamuzi mbaya kuliko kutofanya kabisa. Tatizo tulilo nalo, unashindwa kutoa uamuzi kwa sababu ya kuogopa kuwa ni mbaya. Kafanyeni uamuzi hasa unaohusu maslahi ya taifa, utakaosaidia kuokoa shida za wanyonge vijijini," alisema.

**MAAGIZO MAZITO**

Katika hotuba yake hiyo aliyoitoa baada ya kuwaapisha, Rais aliwapa maagizo mazito kila waziri huku akimtaka Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, kufanya kazi kwa kutumia taaluma yake ya sheria kwa sababu serikali inataka fedha.

"Siyo kila siku unachukua ndege za TANAPA (Shirika la Hifadhi za Taifa) Tanzania), unakwenda kustarehe, tunataka kazi," alisema.

Katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, amewarudisha William Lukuvi na Naibu Waziri, Angelina Mabula, kutokana na kazi nzuri waliyoifanya katika kutatua migogoro ya ardhi.

Hata hivyo, alisema bado wana kazi kubwa na kuwataka wakafanye mabadiliko kwa kusimamia sekta ya ardhi hasa kuwashughulikia wale wanaowadhulumu wenzao.

**ELIMU**

Alisema amemrudisha katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako na kumpa msaidizi mwingine ili wakafanye mabadiliko ikiwa ni pamoja na kulifanya somo la historia kuwa la lazima na lihusu historia ya Tanzania ili kujenga uzalendo.

"Watanzania wajue walikotoka, vijana hawajui historia ya nchi wala mapambano ya baba wa taifa alivyoleta uhuru, ndiyo maana anatumwa mtu aliyepandikizwa na watu wengine yeye kwake ni salama tu, taifa kama Tanzania haliwezi likapendwa wakati lina rasilimali za kutosha," alisema.

**TAMISEMI**

Rais Magufuli alisema Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, (TAMISEMI), Seleman Jafo, amefanya kazi ya kuzunguka lakini ipo changamoto ya matumizi mabaya ya fedha na kumtaka akasimamie.

"Nilifikiria sana kukurudisha au kutokukurudisha, nasema ukweli tuelewane, hili la matumizi ya fedha ni baya, unakuta Mkurugenzi ananunua gari la Sh. milioni 400.

"Tumeangaika kuzipata fedha za kurejesha huduma kwa jamii (CSR), wananchi wanachangishwa madawati hayajatosha halafu mtu anazitumia. nataka kazi ya kwanza (Jafo) ukamsimamishe Mkurugenzi wa Geita na utume watu wakafanye uchunguzi, badala ya kununua madawati unanunua gari, Mkuu wa Mkoa (RC) hana gari kama hilo la Mkurugenzi," alisema.

**MADINI**

Alisema bado madini yanayochimbwa yanatoroshwa na kutolea mfano katika mgodi wa Chunywa ambako yanapelekwa nchi za jirani na Tanzanite inayochimbwa Mirerani nayo baadhi ya watu wanapita nayo.

**MAWASILIANO**

Alisema anafahamu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambayo waziri wake ni Dk. Faustine Ndugulile, ni daktari wa binadamu na naibu wake, Kundo Mathew ni mhandisi katika TEHAMA.

"Ni mchanganyiko mzuri tutaangalia hata Katibu Mkuu tutakayempeleka huko naye awe na maarifa hayo, ninataka wizara hii ifanye kazi kwa sababu ndio usalama wa nchi, watu wanacheza wanavyotaka," alisema.

**KILIMO**

Rais Magufuli alisema Waziri wake, Prof. Aldoph Mkenda, ambaye amesomea uchumi amemtaka akaifanyie kazi taaluma yake kwenye kilimo kilichoajiri zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania.

**UJENZI**

Alimweleza waziri wake, Dk. Leonard Chamuriho, aliyekuwa Katibu Mkuu Uchukuzi, kuwa akiwa kwenye nafasi hiyo alisimamia TRC, TCAA na rada ikanunuliwa, viwanja vya ndege vikajengwa na waliagiza meli, sasa akasimamie miradi mikubwa ikakamilike.

**UWEKEZAJI**

Rais Magufuli alimweleza Prof. Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Uwekezaji, kuwa hakufanya vizuri Wizara ya Maji alipokuwa Katibu Mkuu, hivyo amempa wizara hiyo akazungumze na wawekezaji wa ndani na nje ili waje wengi na ndani ya siku 14 wapate kila kitu.

**AFYA**

Alimtaka Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, na naibu wake, wakaendeleze yaliyofanyika.

"Ninajua ulipokuwa Naibu Katibu Mkuu ulikuwa unakwamishwa na Katibu Mkuu wako na walio juu. Ukitoa oda wanakwambia hapana. Tumekupeleka ukawe waziri ukatoe oda ya kweli, hatutaki Tanzania iwe sehemu ya majaribio kila chanjo tunamezea tu. Kasimamie maadili na kulinda maslahi ya Watanzania," alisema.

**MIFUGO**

Aliwataka waziri na naibu wake wakadhibiti uvuvi haramu na wakalinde maslahi ya wafugaji na wavuvi kwa kuwatengenezea maeneo, wakaanzishe viwanda vingi vya nyama na maziwa ili sekta hizo zichangie pato la taifa.

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

Alimweleza Jenista Muhagama ambaye ni Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, kuwa mambo ya sera alifanya vizuri, lakini upande wa kazi hayakuwa mazuri kwa kuwa kuna wageni waliokuwa wakipewa vibali vya kazi wakati wazawa wenye sifa wapo.

MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MKOA WA GEITA

GEITA

MADAI NA. 22 YA MWAKA 2020

TUBETI NYAMHANGA.................. MDAI NA. 1
JOHN NDEGE.................. MDAI NA. 2

VERSUS

NICHOLAUS NYALUSAHI.................. MDAIWA NA. 1
REONARD ZAMBELI.................. MDAIWA NA. 2
ZAKARIA NYAMHANGA.................. MDAIWA NA. 3

Kwa

1. NICHOLAUS NYALUSAHI
2. REONALD ZAMBELI

**KUITWA SHAURINI**

Mnaarifiwa kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe 15/12/2020, kuja kusikiliza shauri la madai yaliyofunguliwa na wadai dhidi yenu.

Mnatahadharishwa kuwa endapo hamtofika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa maamuzi.

Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo hii tarehe 1 /12/2020.

RESIDENT MAGISTRATE
GEITA
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MKOA
GEITA

KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DAR ES SALAAM

UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI

MIRATHI No. 86 YA MWAKA 2020

MAOMBI YA BARUZA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU
FERNANDO MORALES

MWOMBAJI/WAOMBAJI
CREMILDA FERNANDO COSSA MORALES

TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 15 Mwezi wa February, 2021.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 07 Mwezi wa December, 2020.

NAIBU MSAJILI

# Akosa uwaziri baada ya kushindwa kusoma kiapo



Naibu Waziri mteule wa Madini, Francis Ndulane Kumba, akiteremka kutoka jukwaa kuu, baada ya kushindwa kusoma kiapo mbele ya Rais John Magufuli, Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ALIYEKUWA Naibu Waziri mteule wa Madini katika Baraza la Mawaziri lililotangazwa Desemba 5, mwaka huu, Francis Ndulane, jana alishindwa kusoma kiapo mbele ya Rais Magufuli.

Hatua hiyo imesababisha kupoteza nafasi hiyo na Rais amesema atateua mtu mwingine kushika wadhifa huo.

Tukio hilo lilitokea jana Ikulu, Chamwino wakati wa mawaziri na manaibu wao kula kiapo. Ndulane, baada ya kupewa karatasi ya kiapo pamoja na Biblia Takatifu, alijikuta akishindwa kusoma kwa mtiririko na aliposoma baadhi ya maneno hakuyamalizia.

Kutokana na kushindwa kusoma kiapo hicho kwa ufasaha zaidi ya mara tatu, aliondolewa kwenye eneo la kula kiapo na kurudi katika eneo alilokuwa ameketi awali.

Baada ya kumaliza kuwaapisha mawaziri hao na kula kiapo cha maadili, Rais Magufuli alisema atamchagua mtu mwingine atakayechukua nafasi hiyo.

"Hapa kila mmoja wenu namfahamu sana tu. Hata wewe ambaye umeshindwa kuapa hii nafasi yako tutahakikisha tunachagua mtu mwingine atakaye 'fit' (tosha) na anayeweza kusoma kiapo vizuri maana yake hii inaonyesha kuwa hapa tunaweza hata kuchomekewa watu wasiofaa," alisema.

Kutokana na kushindwa huko, Rais Magufuli alisema pia watamfanyia uchunguzi kubaini vyeti vyake vya elimu kama ni halali kwa kuwa elimu yake na alivyofanya ni vitu viwili tofauti.

"Kama unashindwa kusoma kiapo kweli utaweza kusoma mikataba yenye maslahi na taifa letu kwenye madini ambako kumekuwa na mikataba mikubwa? Ni lazima tukufanyie uchunguzi kwenye hiyo Masters yako sayansi (Shahada ya Uzamili) ya Finance (fedha)," alisisitiza.

Vile vile, katika viapo, pia Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mwanaidi Ali Khamis, alilazimika kusoma kiapo chake zaidi ya mara nne kutokana na kukosea na kuamuliwa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, kurudia.

Khamisi alikosea kusoma kiapo chake kutokana na kutamka maneno ambayo hayakuwamo katika kiapo na kuongeza mengine.

Katika kiapo chake, ambayo alikuwa akiyaongeza ni badala ya Baraza la Mawaziri alikuwa akisema Baraza la Mapinduzi.

Hata hivyo, Rais Magufuli alisema anaonekana suala la mapinduzi limemjaa moyoni kwa sababu amekuwa na kuishi katika mapinduzi hayo.

# Sababu Ummy kwenda Ofisi ya Makamu wa Rais

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ametaja sababu ya kumhamisha Ummy Mwalimu kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwenda kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Katiba Baraza la Mawaziri lililopita, Ummy alikuwa mmoja wa mawaziri wachache waliodumu katika wizara moja katika miaka yote mitano ya ngwe ya kwanza ya Rais Magufuli.

Mawaziri wengine ni Dk. Philip Mpango (Fedha na Mipango), William Lukuvi (Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi), Prof. Joyce Ndalichako (Elimu, Sayansi na Teknolojia), Jenista Mhagama (Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana na wenye Ulemavu) na Dk. Hussein Mwinyi (Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa) ambaye sasa ni Rais wa Zanzibar.

Pia katika naibu mawaziri, waliodumu kwa miaka mitano kwenye nafasi moja ni Anthony Mavunde (Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana), Dk. Angelina Mabula (Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi), Hamad Yussuf Masauni (mambo ya Ndani ya Nchi) na Dk. Ashatu Kijaji (Fedha na Mipango). Katika orodha hiyo, Dk. Mabula pekee ndiye aliyerejea katika nafasi yake huku wengine wakiachwa.

Akizungumza jana mjini Dodoma baada ya kuwaapisha mawaziri na naibu mawaziri, Rais Magufuli alisema Ummy alifanya kazi nzuri katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hasa katika kupambana na corona.

Rais alisema katika Ofisi ya Makamu wa Rais, hasa Mazingira, kulikuwa na kulegalega, hivyo ameona ampeleke huko ili akarekebishe mambo.

"Tukaona ofisi ya Makamu wa Rais inalegalega, sasa tukaona aende huko nako akanyooshe kama alivyofanya Wizara ya Afya.

"Juzi tumeshika zaidi ya magari manane yanasomba vyuma chakavu wakati ni malighafi zinazotumika kujengea reli ya Standard Gauge (SGR) na Narrow Gauge yetu vinachukuliwa, vinapita, vinakwenda kutengeneza nondo.

"Baadhi ya polisi wachache akiwamo Mkuu wa Kituo cha Mlandizi, Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD) na watendaji wake wanahusika, ninaamini IGP umeshawatoa," alisema.

Rais Magufuli alisema serikali inatumia zaidi ya Sh. trilioni saba kujenga reli, halafu Watanzania wengine wanasomba kwa ajili ya fedha kidogo ili kuuza kwenye viwanda vya nondo.

"Ndiyo maana nimekuchukua Ummy Mwalimu na Mwita (Waitara) ambaye atakuwa anatoa amri za Kikurya, mkafanye kazi huko," alisema.

# JPM ataja sababu za kuteuliwa wazee

**Na Romana Mallya**

SABABU za kuteuliwa wazee katika Baraza la Bawaziri zimeelezwa kuwa ni kuweka uwiano, kupata ushauri na kumwongoza Rais katika mambo mbalimbali ya uongozi.

Baraza hilo jipya litakalofanya kazi ya kumsaidia Rais kwa awamu ya pili ya miaka mitano, lenye mawaziri 21 na naibu mawaziri 22.

Akizungumza jana mjini Dodoma muda mfupi baada ya kuwaapisha mawaziri na naibu mawaziri hao Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma, Rais John Magufuli alisema hiyo ndiyo sababu ya kuchanganya vijana na wazee katika baraza hilo.

"Ndiyo maana tumeweka uwiano hata wazee wapo. Kapteni George Mkuchika (Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), tangu utawala wa Mwalimu Julius Nyerere, awamu ya pili ya Ali Hassan Mwinyi, awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, awamu ya nne, Jakaya Kikwete alikuwapo na awamu hii yupo.

"Mkuchika ana miaka 72, hivyo lazima tubakishe kumbukumbu za kitaasisi kwenye taifa hili. Kwenye Baraza la Mawaziri, ninahitaji wazee wa kunishauri na kuniongoza hapa umekwenda vipi," alisema.

Rais alisema alimteua Mkuchika kwa upendo huo na kwa sababu ni mzee na baraza linahitaji wazee pia.

Alisema kila wizara walichambua na kuwaeleza kuwa si kwamba walioteuliwa ni wazuri sana, bali vipo vidosari ambavyo anaamini watavirekebisha kwa sababu yalipita si ndwele.


NORWEGIAN CHURCH AID
actalliance

**SECTION I – INVITATION:**

**Tender No. 02/NCA-T/MuS/2020 FOR CONSTRUCTION OF TOWER AND INSTALLATION OF SIX SOLAR POWERED WATER SYSTEMS WITHIN MBULU AND HANANG DISTRICTS – DECEMBER 2020 TO FEBRUARY 2021**

1. Norwegian Church Aid (NCA) is a Norwegian non-governmental and development organization working to promote Social Justice, Human Rights and Economic Justice for poor communities. The NCA has its foundations based in a congregation of churches in Norway, whose efforts are dedicated towards eradicating poverty, its causes and social deprivation. In Tanzania, NCA works with poor communities and local partners in 36 districts.
2. NCA – MuS Project in Tanzania invites electronic bids from eligible and qualified registered Contractors for **CONSTRUCTION OF TOWER AND INSTALLATION OF SIX SOLAR POWERED WATER SYSTEMS WITHIN MBULU AND HANANG DISTRICTS – DECEMBER 2020 TO FEBRUARY 2021.**
3. Bidding will be conducted through electronic procedures and to be opened to eligible registered Bidders and will be conducted as per NCA Procurement Policy.
4. Interested eligible bidders may obtain further information from **NCA Tanzania procurement committee, Email:** procurement.tanzania@nca.no from **08:30am to 16:00pm** on Monday to Friday from **10th – 15th December 2020** inclusive except on public holidays.
5. Qualification requirements include legal status i.e. CRB's registration Contractor in Construction Works, should have qualified and experienced key personnel for administration and execution of the contract, proposed sub-contractors and firms involved (if any) and sound financial status of the bidder(s)
6. Norwegian Church Aid will not accept hard copy of tender documents, therefore all bids should be scanned in one original document in PDF format and sent to procurement.tanzania@nca.no and shall be submitted on or before Monday ***21st December 2020 at 16:00 pm Tanzanian local time. Late bids, incomplete of bids, hard copy bids, bids not received in the email, and not read out through digital meeting will be rejected.***

   All bids will be opened electronically through digital meeting on ***Tuesday 22nd December 2020 at 14:00p.m*** by NCA Procurement Committee for read out and evaluation exercise. ***A link for this meeting will be shared to all bidders on Monday 21st December 2020 by 10.00am***
7. All bids and their supporting documents such as solar power scheme design sheets shall be accompanied by a bid securing declaration form in the format provided in the tender documents
8. Norwegian Church Aid is not bound/Obligated to accept the lowest/Highest bid or any of the bids
9. All bidders must attach detailed CVs for technical and non- technical team, list of equipment, list of all similar activities carried out for the past five years to date and legal certificates including bank statements
10. A financial bank statement of the company with official document proving that the person signing on behalf of the Construction company is duly authorised to do so, scanned copies of original documents defining the constitution or legal status, place of registration, and principal, place of business
11. Experience as prime contractor in the boreholes drilling and installation work of at least two projects of a similar nature and complexity equivalent to the Works under this Tender undertaken within the last 5 years (to comply with this requirement, works cited should be at least 70 percent complete and at least one project should be 100% completed and fully operational)
12. The essential equipment such as Concrete Mixer, 4W drive truck for transporting construction materials, at least one 4W-drive supervision vehicle and other essential tools to enable successfully installation of all works to be made available for the Contract by the successful Bidder
13. Evidence of adequate working capital for this contract, Information regarding litigation, current and any other material and information which should be provided and made known to the contracting authority.
14. The minimum required annual volume of construction work for the successful Bidder in any of the last 5 years shall be **Tshs. 250,000,000.00**

# Wamwangukia JPM ukatili wa kijinsia

**Na Joseph Mwendapole**

WANAWAKE wamemwomba Rais John Magufuli kusaidia jitihada za kutokomeza ukatili wa kijinsia, huku wakimpongeza kwa kutokomeza matatizo mengine kwenye jamii ikiwamo ugonjwa wa corona na dawa za kulevya.

Ombi hilo lilitolewa jana na Balozi Getrude Mongela wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo kwa 'machampioni' 16 wa kupinga ukatili wa kijinsia walio mstari wa mbele kutetea haki za wanawake na mtoto wa kike.

Tuzo hizo ziliandaliwa kwa pamoja na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na Ubalozi wa Denmark kwa ajili ya kuwatambua watu waliofanya vizuri zaidi kwenye harakati za kupinga ukatili wa kijinsia.

Mongela alisema anaamini kwa dhati kwamba Rais Magufuli anaweza kumaliza matatizo yanayowakabili wanawake hasa ubakaji kwa kuwa amefanya mambo makubwa ambayo watu wengi hawakuwa wanatarajia kama kutoa elimu bure na kujenga miundombinu imara.

"Mtu aliyeweza kutoa elimu bure kwa watoto wa Watanzania, aliyetokomeza COVID-19, mimi namwamini ni msikivu sana. Tumwombe tumwambie kama umeweza haya makubwa na hili dogo pia analiweza. Naamini atatusaidia sisi tutimize wajibu wetu kama wanawake," alisema Mongela.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, ambaye ni miongoni mwa machampioni waliopewa tuzo hizo, alisema alipoteuliwa tu mwaka 2016 alianza kupambana na vitendo vya mauaji ya wanawake wazee walioonekana kuwa na macho mekundu na alifanikiwa.

"Nilipoteuliwa tu nilisema sitalala mpaka nitokomeze mauaji haya ya vikongwe na kwa kweli tulijipanga mimi na Mkuu wa Jeshi la Polisi Mkoa tumefanikiwa hivi sasa Shinyanga ni salama kwa uwekezaji makazi na huwezi kusikia tena mauaji ya wanawake wazee," alisema.

Kuhusu mimba za wanafunzi, Telack alisema walifanya kampeni kubwa kuwakamata waliokuwa wakioa au kuozesha wanafunzi na hivi sasa idadi kubwa ya wanafunzi wa kike mkoani humo wanahitimu masomo bila kupata ujauzito.

Alisema yeye na timu yake walifanya kampeni ya kuchunguza kila harusi inayofanyika mkoani humo na wanapokuta anayeoa au kuolewa ni mwanafunzi, waliwachukua wote waliokuwa wanahusika kwenye sherehe hizo na kuwafikisha kwenye vyombo husika kwa hatua zaidi.

"Tulikuwa tunapita shuleni kuangalia mahudhurio ya nani hayupo, yuko wapi na anafanya nini. Tuliwafuatilia wote tukahakikisha walioacha shule wanarudi na wale waliopanga kuolewa tulivuruga mipango yao na sasa wengi wako shuleni wanaendelea na masomo," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa WiLDAF, Anna Kulaya, alisema tuzo hizo ambazo zimezinduliwa mwaka huu zitakuwa zikifanyika kila mwaka kwa ajili ya kuwatambua watu waliofanya vizuri zaidi kwenye mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia

Alisema kuna ukatili mwingi unaotokea kwa wanawake ukiwamo ubakaji kwa wanawake na wasichana ndiyo maana mwaka huu WiLDAF imeamua kuangalia pia jitihada zinazofanywa na watu wa kawaida kabisa kupambana na ukatili wa kijinsia na kupata mafanikio.




Balozi wa Denmark hapa nchini, Mette Dissing (kulia), akiwa na baadhi ya washindi wa tuzo ya kupinga ukatili wa kijinsia katika hafla ya utoaji tuzo kwa 'machampioni' 16 wa kupinga ukatili, jijini Dar es Salaam. Wa (pili kulia) ni Mwanzilishi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Dk. Judith Odunga. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TMA yataja chanzo ongezeko la joto

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imesema ongezeko la joto katika baadhi ya maeneo nchini linatokana na jua la utosi kuwa kwenye kizio cha kusini mwa dunia Tanzania ikiwa sehemu mojawapo.

Taarifa ya mamlaka hiyo imesema hali hiyo itaendelea hadi mwanzoni mwa Machi, mwakani.

Kwa kawaida, kwa mujibu wa taarifa hiyo, kipindi cha Oktoba hadi Machi, kila mwaka, jua la utosi linakuwa katika maeneo ya kizio cha kusini mwa dunia. Tanzania ni moja ya nchi zilizoko katika kizio cha kusini na hali ya joto huwa kubwa katika maeneo mengi ikilinganishwa na miezi mingine.

Taarifa hiyo pia ilisema kwa Tanzania vipindi vya jua la utosi vinafikia kilele mwishoni mwa Novemba wakati jua la utosi likiwa linaelekea kusini (Tropiki ya Kaprikoni) na hali hiyo hujirudia tena Februari wakati jua la utosi likiwa linaelekea kaskazini (Tropiki ya Kansa).

"Jua la utosi huambatana na hali ya joto kali kwa sababu kipindi hicho ndicho uso wa dunia katika eneo tajwa huwa karibu zaidi na jua kuliko maeneo mengine. Nyakati za usiku pia kunaonekana kuwa na hali ya joto kutokana na kuwapo kwa kiwango kikubwa cha unyevunyevu angani kinachofikia asilimia 80 na zaidi kwa baadhi ya maeneo," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Aidha, unyevunyevu huo, kwa mujibu wa taarifa hiyo, hutunza hali ya joto litokanalo na mionzi ya jua na hivyo kuleta hali ya fukuto.

"Katika kipindi hiki cha mwezi Desemba, 2020 upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo yanayopata mvua za vuli (ukanda wa Ziwa Victoria, Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki pamoja na Pwani ya Kaskazini)," ilibainisha taarifa hiyo.

Imeelezwa hali hiyo inatarajiwa kuendelea kusababisha uwepo wa hali ya joto katika maeneo hayo.

Hata hivyo, taarifa ilisema hali ya joto inatarajiwa kupungua kidogo katika kipindi cha Januari kutokana na mvua zinazotarajiwa katika baadhi ya maeneo na kwamba vipindi vya joto vinatarajiwa kuendelea kuongezeka Februari wakati jua litakapokuwa la utosi nchini.

"Baada ya kipindi hicho hali ya joto inatarajiwa kuanza kupungua hasa kuelekea Machi. Mtawanyiko wa mvua unatarajiwa kuongezeka katika maeneo yanayopata mvua za msimu na kuanza kwa msimu wa mvua za masika," taarifa hiyo ilisema.

Pia mamlaka hiyo imesema inaendelea kufuatilia mwenendo wa joto na taarifa zake zitatolewa kwenye utabiri wake wa kila siku.

# Lori la mafuta labambwa na bangi, bunduki yakamatwa kwenye miwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro limekamata lori la kusafirisha mafuta likiwa limepakia viroba 81 vya bangi na kuvihifadhi ndani ya vyumba vitupu vya kuhifadhi mafuta.

Lori hilo limekamatwa likitokea mkoani Mara kwenda jijini Dar es Salaam na kwamba dereva wa lori hilo, ametoroka na anatafutwa na polisi.

Wakati lori hilo linanaswa, polisi wamemkamata Mawazo Sospeter, mkazi wa Mbingu wilayani Kilombero, akiwa na bunduki aina ya rifle 458 yenye namba 42599 bila kibali na silaha hiyo aliifunga kwenye kiroba kwa kuichanganya na miwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Fortunatus Musilimu, alisema jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Hilo ni tukio la kwanza kwa kamanda huyo kukutana nalo tangu kuteuliwa kushika nafasi hiyo akitokea kuwa Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini.

Musilimu alisema lori hilo lenye namba za usajili T 486 DSU lenye tela namba T 275 BXB aina ya Hongvan, mali ya MC Soud Industry LTD ya mkoani Shinyanga, lilikamatwa Desemba 06, majira ya saa 5:00 asubuhi, maeneo ya Morogoro Junior Seminary, Manispaa ya Morogoro katika barabara kuu ya Morogoro - Dar es Salaam.

"Kutokana na upekuzi mkali wa magari uliokuwa ukifanywa na askari, dereva wa lori alilitelekeza barabarani na kutoroka. Viroba hivyo vilikuwa vimewekwa kwenye vyumba vya kuhifadhi mafuta," alisema Musilimu.

Kamanda huyo alimtaka dereva huyo kujisalimisha polisi kabla hatua kali dhidi yake kuchukuliwa, sambamba na kumtaka mmiliki wa lori hilo kufika kituo kikuu cha Polisi Morogoro kwa mahojiano zaidi. Wakati akitamka hayo, Musilimu alisema jitihada zaidi kumsaka dereva na mtandao wa watu wanaohusika na usafirishaji wa bangi unaendelea.

Pia alisema wamewakamata watuhumiwa wa uhalifu 31 wakiwamo wanaodaiwa kuwa wazoefu, wawili walioachiwa gerezani na kuendelea na uhalifu, sambamba na wengine ambao hufanya uhalifu na kukimbilia nje ya Morogoro.

Miongoni mwa waliokamatwa katika operesheni maalum iliyofanyika Desemba Mosi, mwaka huu, Musilimu alisema ni watuhumiwa waliokuwa wakijihusisha na usafirishaji wa bangi, uuzaji wa pombe haramu ya gongo, unyang'anyi, uchezaji wa kamari, kuiba vyuma kwenye miundombinu ya reli, barabara na mauaji.

Katika operesheni hiyo, alisema wamekamatwa vijana wawili mapacha wenye umri wa miaka 19, Justine Mapunda, Joseph Mapunda, wakazi wa Sultani Area mjini Morogoro ambao baada ya kuachiwa gerezani kwa makosa ya mauaji, wameendelea kujihusisha na uhalifu ikiwamo matukio ya mauaji na unyang'anyi wa kutumia silaha.

## TANGAZO



itel
JAZA TUKUJAZE TENA
Hata ukinunua SIMU!
Nunua itel T20 au Kitochi 4G Smart
Pata GB30 BURE Mwaka mzima
Shinda PIKIPIKI na SMART TV
Kibao kila wiki
4G+
tigo
itel T20 kwa Tsh. 84,900/- au TECNO Kitochi 4G Smart kwa Tsh. 45,000/-
Tembelea maduka ya Tigo nchi nzima. Kwa vigezo na masharti tembelea www.tigo.co.tz

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watoto wapewe vitamin A kuwaepushia madhara

**TAARIFA** kuwa upungufu wa vitamin A bado ni tatizo nchini, zinapaswa kuchukuliwa kwa umuhimu mkubwa ili kupunguzwa ukubwa wake.

Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), ndiyo iliyobainisha hayo kwa kueleza kwamba moja ya matatizo makubwa ya lishe nchini ni upungufu wa vitamini A.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi, Chakula na Lishe, Dk. Elifatio Towo, alitoa kauli hiyo juzi jijini Dar es Salaam alikokuwa akifungua semina ya waandishi wa habari kuhusu mwezi wa afya na lishe ya mtoto.

Alisema bado elimu inatakiwa kwa jamii ili kuhamasisha wananchi kutumia vyakula vyenye vitamini A kwa watoto, ili kuepukana na matatizo ya lishe duni.

Alisema kwa mujibu wa utafiti wa afya na mgawanyo wa watu wa mwaka 2010, takribani asilimia 33 ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano walibainika kuwa na upungufu wa vitamini A mwilini.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo wa lishe, upungufu wa vitamini A mwilini husababisha madhara mengi kwa mtoto ikiwamo ukosefu wa kinga mwilini, hivyo mtoto kuwa katika hatari ya kupata magonjwa mara kwa mara, kutoona vizuri katika mwanga hafifu.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo kuna hatua madhubuti zinapaswa kuchukuliwa ili kudhibiti tatizo la upungufu wa vitamini A.

Kutokana na ukubwa huu wa tatizo la vitamini A, tunaona kuwa sasa ni wakati mwafaka wa kuchukuliwa hatua za kulipunguza kama si kulimaliza kabisa.

Pamoja na hatua ambazo serikali imekuwa ikizichukua na inaendelea kuzichukua katika kukabiliana na tatizo hilo, tunashauri kuwa jitihada zaidi zichukuliwe kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Wakati huu jamii yetu hainabudi kubadilika na kuachana na mawazo mgando kwamba kila kitu lazima kifanywe na serikali. Zama hizo zimepita.

Katika dunia ya leo kila mmoja anawajibika kutoa mchango wake. Ndio maana mambo yanafanywa kwa kushirikisha wadau.

Kama kila kitu jamii itakiacha kifanywe na serikali, taifa letu litachelewa kufika katika uchumi mkubwa. Serikali ina majukumu mengi ya kutekeleza.


Hata hivyo, tunapongeza hatua kadhaa ambazo zinachukuliwa katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa vitamin A, ikiwamo kuwapo mwezi wa afya na lishe ya mtoto. Mkakati huu lengo lake ni mojawapo ya mikakati ya kulinda afya na maendeleo ya mtoto, ambapo katika kipindi hiki huduma jumuishi za afya na lishe hutolewa kwa mtoto mwenye umri kuanzia miezi sita hadi miaka mitano.

Mkakati huo ni mzuri kwa kuwa Dk. Towo anasema huduma wanazozitoa ni kutoa matone ya vitamini A, utoaji wa dawa za kutibu maambukizi ya minyoo, upimaji wa hali ya lishe, utoaji wa ushauri nasaha na kutoa rufani kwa mtoto anayebainika kuwa na utapiamlo mkali.

Huduma hizi zikiboreshwa zaidi, ni imani yetu kwamba zitawafikia watoto wengi zaidi ambao ndio walengwa. Tunasema hivyo kutokana na maelezo ya Dk. Towo kwamba hutolewa kila baada ya miezi sita yaani mwezi Juni na Desemba kila mwaka na kuwafikia watoto wengi zaidi.

Kwamba takribani watoto 8,674,656 walifikiwa na huduma zinatolewa katika mwezi wa afya ya moto, mwezi Desemba mwaka 2019.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Irene Philemon

# Tujipige marufuku unyanyasaji kijinsia, tunachoamua kishibe stadi za busara

**MAADHIMISHIO** ya Siku 16 za Mapambano dhidi ya Ukatili wa Kijinsia nchini na duniani kote yanafika kileleni.

Lengo ni kukabiliana na madhila ya kijamii, pia madhara yanayotokana na tabia zetu ambazo zikiangaliwa kwa kina, ni zao la uamuzi wa binadamu.

Nadiriki kujuta; binadamu, binadamu binadamu! Mbona mnatenda yasiyowafaa wenzenu? Nifafanue kidogo kwamba tunaowanyanyasa wana haki kamili ya kuishi na kufurahia maisha.

Pia, nawatamkia enyi watu mnaofanya unyama wa kuwakatili wenzenu kufurahisha au kwa manufaa ya nafsi zenu, hakikisheni mnabadilika kwa kuacha haya; msiwaumize kisaikolojia, kuwavunja moyo na kuhisi wao hawana haki ya kuishi.

Niseme, kinababa na kinamama mhakikishe hamfanyi unyama. Tunajua wanawake ndio wamekuwa wanafanyiwa zaidi vitendo hivyo vya ukatili vilivyokithiri, kunyanyapaliwa na kudharauliwa, kunyimwa haki zao za msingi, pia kunyanyaswa.

**Niseme, kinababa na kinamama mhakikishe hamfanyi unyama. Tunajua wanawake ndio wamekuwa wanafanyiwa zaidi vitendo hivyo vya ukatili vilivyokithiri, kunyanyapaliwa na kudharauliwa, kunyimwa haki zao za msingi, pia kunyanyaswa.**

Kinachopaswa kufanyika mahali hapo ni kwamba kila panapoonekana uonevu wa aina yoyote, hatua za kisheria zinapaswa kuchukuliwa kuanzia mzizi wa mahali umma unaoshuhudia, ili kuwa funzo kwa wengine wenye taiba hiyo.

Sambamba na hilo, nanyi mnaotendewa hayo, msingi mkuu unatakiwa kutolewa taarifa haraka kwa mamlaka zinazohusika. Inakuwa njia sahihi inayowawezesha kujenga mazingira ya kusaidiwa.

Na kama hata binafsi mnapoona kwamba hilo hamuwezi kulifanya au kulifanikisha, ni vyema kuomba msaada wa majirani kuwafanikishia majukumu hayo ya kujikomboa kwa kuwasiliana na dola kuu inayosimamia sheria za nchi.

Pia, nithubutu kuwageuzia uso wanaopokea taarifa hizo kwamba, pale inapotokea hamzitendei haki inakuwa jambo baya sana. Msipuuze taarifa hizo, kwani hamjui mlalamikaji ana maumivu ya kiwango gani.

Kufuatilia taarifa za kisheria kutoka hatua ya awali ya malalamiko ya jinai ya unyanyasaji, kufanya hivyo kuna tafsiri huenda zaidi ya kile mnachokiona. Tayari mnakuwa katika mkondo wa kumsaidia aliyetendewa na jamii nzima kwa jumla.

Lakini, tunapojiuliza kwanini yote hayo yanatokea, jibu linaanzia tafsiri kwamba, katika maisha ya mwanadamu kuna namna na wakati sahihi wa kufanya uamuzi.

Binadamu anapofikia hatua ya kuamua, ni vyema akahakikisha unaangukia usahihi, kwani vinginevyo ataangukia kupotoka.

Si rahisi mwanadamu kuwa na ubashiri sahihi, kujua atafurahishwa au kuudhiwa katika muda fulani. Mazingira ambayo binafsi huwa naupa tafsiri moyo ukiwa umetulia, ndio muda sahihi na mzuri kuamua kwa mtazamo chanya.

Sababu kuu ni kwamba, moyo una kawaida ya kukinzana na usahihi unapokwazika, wakati wa kuamua. Ni kanuni ambayo mtu anapaswa kuwa nayo, anapogundua amekwazika asifanye uamuzi, kwani inamwingiza katika hatari ya kubomoa, badala ya lengo la msingi, kujenga.

Wanadamu wengi huwa tunaangukia makosa ya kufanya uamuzi ama wakati tuna furaha iliyopitiliza au huzuni kubwa, ambayo ina kawaida ya kuangukia majuto katika maisha ya baadaye, kama waswahili wanavyotafsiri, 'majuto ni mjukuu' kwa maana hujitokeza baadaye.

Ni aina ya uamuzi unaompeleka mtu pabaya na hata kumpotosha kabisa. Ili kuamua kwa usahihi, mtu anapaswa kujiuliza maswali makuu manne.

Hapo kuna muda gani mtu anafanya uamuzi? Je, anachoamua huwa kina faida au hasara? Kama yana hasara, unachukua hatua gani kuyarekebisha? Iwapo faida, ulipata faida na maendeleo gani?

# Maadhimisho ya siku ya Haki za Binadamu kitaifa

**Na Anna Henga**

**Utangulizi**

Kituo cha sheria na Haki za binadam (LHRC) leo Desemba10 mwaka 2020 tunaadhimisha siku ya kitaifa ya Haki za Binadam katika ukumbi wa Golden Jubilee posta jijini Dr es Saaam. Maadhimisho haya yatafuatiwa na hafla ya utoaji wa Tuzo za Majimaji.Kauli mbiu katika maadhimisho haya inasema; **Haki ni maendeleo simamia Haki**.Nchini Tanzania upo umuhimu mkubwa sana wa kushiriki katika maadhimisho ya siku ya Haki za Binadamu kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatambua haki za binadam na inaweka bayana wajibu wa kila mtu katika kulinda na kuheshimu haki za binadam katika ibara ya 12 hadi ya ile ya 32.

Itakumbukwa kwamba mnamo tarehe 10 Desemba 1948 ilitangazwa Azimio na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa juu Tamko la Haki za Binadamu na tangu mwaka 1950 ikaanza rasmi kufanyika siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu. Kiini cha Siku hiyo ni kuelimisha na kuhamasisha watu kulingana na binadamu alivyo na kukumbusha hatua zilizopigwa na jamii katika kutekeleza sula la heshima ya binadamu wote, dhidi ya utumwa na kukandamizwa kwa haki binafsi. Hiyo haijalishi kama mtu ni mwanaume, mwanamke, au mtoto, awe anazungumza lugha yoyote iwe kiswahili, Kichina au Kijerumani; haijalishi una rangi ya ngozi Njano, Nyeupe kama theruji au Nyeusi, kila mtu anayo haki ya kuwa binadamu aliyezaliwa huru na sawa, mwenye hadhi na haki sawa. Tamko hili lina Ibara 30, ambapo ibara ya kwanza ya tamko hilo inaeleza wazi kuwa, "Watu wote wamezaliwa huru hadhi na haki zao ni sawa wote wana akili na wana dhamiri hivyo yapaswa watendeane kwa usawa. Kadhalika zipo ibara zinazohusu raia, siasa, uchumi, kijamii na utamaduni ambapo inazuia kabisa kutesa na hali isiyostahili kwa wafungwa, haki sawa na mchakato sawa, bila kushutumu.Vilevile ibara inayohusu haki ya uzalendo na uhuru wa kuzunguka kwa binadamu mahali popote kwa kuzingatia sheria zilizowekwa.

**Kupinga ukatili dhidi ya wanawake Tanzania**

Nchini Tanzania kundi la wanawake limekuwa likikumbana na unyanyasaji wa aina tofauti tofauti kama kunyimwa haki ya kumiliki mali pamoja na ukatili wa kijinsia.Tunapofanya maadhimisho ya kitaifa ya siku ya haki za binadam tunakamilisha pia kampeni ya siku 16 ya kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto ambapo kwa kipindi cha siku 16 kauli mbiu imekuwa ni ***"tupinge ukatili wa kijinsia mabadiliko yanaanza na mimi"*.**

Kwa mujibu wa ripoti ya Haki za Binadam iliyolewa na kituo cha sheria na haki za binadam nchini Tanzania Ukatili dhidi ya wanawake umeongezeka suala ambalo linahitaji kupatiwa ufumbuzi.Ripoti hii inaeleza kuwa pamoja na juhudi mbalimbali zilizofanywa na kuendelea kufanywa, ukatili dhidi ya wanawake, hususan ukatili wa kimwili na kingono, umeendelea kuwa kikwazo kikuu katika ufurahiaji na utekelezaji wa haki za wanawake nchini Tanzania. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2017 hadi mwezi Juni 2019, jumla ya matukio 88,612 ya ukatili wa kijinsia yameripotiwa katika vituo mbalimbali vya polisi. Kwa mwaka 2019, katika kipindi cha mwezi Januari hadi mwezi Juni 2019, jumla ya matukio 3,709 ya ubakaji wa wanawake na watoto yaliripotiwa katika vituo vya polisi nchini. Mkoani Kigoma, mwaka 2019 pia ulikuwa wenye changamoto kubwa kwa wanawake ambao walifanyiwa ukatili wa kingono na kikundi cha wabakaji kilichojiita 'Teleza.' Taarifa mbalimbali na uchunguzi uliofanywa na LHRC na wadau wengine vinaonesha kwamba kikundi hichi cha wabakaji kilikuwa kinawavamia wanawake katika nyumba wanazoishi kisha kuwabaka, na wanawake wengine walibakwa zaidi ya mara moja. Kiongozi wa kikundi hicho alikamatwa mwezi Juni mwaka 2019.

Ripoti ya Haki za binadamu pia inabainisha kuwepo kwa matukio ya Rushwa ya ngono katika ajira, taasisi za elimu ya juu na siasa kama mojawapo ya changamoto kubwa kwa upande wa wanawake. Ripoti ya hivi karibuni ya Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) inaonesha kwamba takribani asilimia 89 ya wanawake katika sekta ya umma wamewahi kufanyiwa ukatili wa kingono wakati wa kutafuta kazi, kupandishwa cheo au kupata huduma. Tasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) iliripoti kwamba inapanga kushirikiana na wadau wengie kufanya utafiti kuhusu rushwa ya ngono katika maeneo na sekta mbalimbali, ikianzia kwenye taasisi za elimu ya juu.

**Mchango madhubuti wa LHRC katika kulinda haki za Binadam Tanzania**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni moja kati ya asasa za kiraia zilizosimama kidete kulinda na kutetea haki za binadam nchini Tanzania, LHRC tunajivunia kuchangia kufanikisha mambo makubwa ya haki za binadamu ikiwemo kuwajengea Watanzania uwezo kuhusu haki za binadamu na sheria. Katika hili tumefanya mambo makubwa yafuatayo;Kutoa elimu ya haki za binadam kupitia vyombo vya habari na kwa njia ya machapisho,Kufanya mafunzo ya kuwajengea uwezo makundi mbalimbali kuhusu umuhimu wa kutambua na kudai haki zao pale zinapopokwa pamoja na kutoa elimu ya kulinda na kutetea haki za binadam. kituo cha sheria na haki za binadam kimefanikiwa kwa kiwango kikubwa kusimamia mchakato wa mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwezesha maboresho muhimu ya sheria na sera mbalimbali nchini Tanzania.

Vilevile kituo cha sheria na haki za binadam kinajivunia kusimama kidete kulinda na kutetea haki za binadam kwa kufungua kesi mbalimbali zinazopinga sheria kandamizi mfano kesi ya Takrima 2005, Biwater 2005, kesi ya Nyamuma 2002, Kesi ya Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari 2019, Kesi ya Mseto 2016, pamoja na Kesi ya Kupinga Sheria ya Ndoa 2016.Vilevile tumeweza kuwajengea uwezo watunga sera na sheria ili kutunga sheria zinazozingatia misingi ya haki za binadamu.

Kwa weledi na uzoefu mkubwa kituo cha sheria na haki za binadam kimeweza kutoa msaada wa kisheria kwa watanzania wasio na uwezo ambapo ni wastani wa watu 15,000 kwa kila mwaka. Kituo kimeweza kuibua matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu na kuonesha hali ya haki za binadamu kupitia tafiti zetu maarufu kama Ripoti ya Haki za Binadamu Tanzania ambayo hutolewa kila mwaka tangu mwaka 2002.Vilevile kituo kimeweza kutetea haki na maslahi ya wafanyakazi nchini Tanzania kwa kuandaa ripoti ya Haki za Binadamu na Biashara.

Kadhalika kituo cha sheria na haki za binadamu kwa miongo miwili kimepata ushindi mkubwa kwa kuweza kuvunja vikwazo vya uwajibikaji miongoni mwa jamii, na mamlaka za usimamizi wa haki nchini Tanzania. Kituo kimeweza pia kusimamia uwajibishwaji kisheria kwa watendaji waliotumia mamlaka yao vibaya katika taasisi binafsi na zile za kiserikali pamoja na kupaza sauti dhidi ya viongozi waliokiuka sheria na haki za binadamu.

**Ulinzi wa Haki kupitia Tuzo za Majimaji**

Katika kuhakikisha ushiriki wa mtu mmoja mmoja ikiwemo wanaharakati wanaokaa mstari wa mbele kulinda na kutetea haki za binadam kituo cha sheria na haki za binadam kilifanikiwa kuanzisha tuzo ya haki za binadamu (Majimaji Awards) ili kutambua uwajibikaji na utendaji uliozingatia misingi ya haki za binadamu na utawala wa sheria. Vilevile katika kuadhimisha siku ya haki za Binadam kwa mwaka huu tuzo hizi zitatolewa kwa washindi watakaokuwa wamepigiwa kura na kuibuka washindi kwa kulinda na kutetea haki za binadam katika namna tofauti tofauti.Tunaamini kuwa Tuzo hizi zitawapatia washindi hamasa kubwa sana ya kuendelea kusimamia haki nchini Tanzania.Mafanikio mengine makubwa ambayo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeweza kuileta jamii pamoja kwa kuanzishwa na kuendelezwa kwa wasaidizi wa kisheria wanaotoa huduma katika Jamii. Hivyo kituo kikaanzisha waangalizi wa haki za binadamu pamoja na kuanzisha kwa vilabu vya haki za binadamu.

**Juhudi za serikali katika kukomesha ukatili dhidi ya wawake na watoto**

Kwa kuwa unyanyasaji na ukatili wa wanawake na watoto unasababisha madhara makubwa katika taifa ikiwemo kukwamisha maendeleo serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania imekuwa ikifanya jitihada ili kukomesha ukatili wa kijinsia.Hata hivyo ukatili wa kijinsia umesababisha kucheleshwa kwa ufikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu wa mwaka 2030. Vilevile kuongezeka kwa matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na wasichana kunahatarisha juhudi za Serikali na wadau wengine za kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu yanayohusiana na usawa wa kijinsia.

Ili kuweza kufikia malengo chanya ya kukomesha ukatili dhidi ya wanawake serikali ya Tanzania kupitia wizara husika ilitenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuondoa Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto 2017/2022. Ingawa uchambuzi wa bajeti iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuondoa Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2019/20 unaonyesha kwamba bajeti inayotengwa haikidhi mahitaji, jambo linaloathiri juhudi za kuondoa ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Uchambuzi unaonyesha kwamba japokuwa bajezi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iliongezeka kwa asilimia 10.7 kwa mwaka 2019/20 ukilinganisha na mwaka 2018/19, bajeti kwa ajili ya Idara ya Maendeleo ya Jamii ilipungua kwa asilimia 1.9, huku bajeti ndogo kwa ajili ya Kitengo cha Ustawi wa Jamii, ambacho kipo chini ya Idara ya Maendeleo ya Jamii, ikipungua kwa asilimia 19.3.Hata hivyo tunaamini kuwa serikali itaendeleza mapambano dhidi ya ukatili wa wanawake na toto.

**Hitimisho**

Kituo cha sheria na Haki za Binadam tunaimani kwamba maadhimisho haya ya kitaifa ya siku ya Haki za binadam yatabakia kuwa hamasa na kumbukumbu kwa wadau wote waliohudhuria.Yote kwa yote napenda kusema kwamba suala la kulinda na kutetea haki ni wajibu wa kila mwana Jamii. Hivyo inampasa kila mmoja wetu kujituma kwa uaminifu na juhudi za dhati ili tuweze kupata maendeleo wakati huo huo tupate jamii yenye haki na usawa. Vilevile nipende kuwatia moyo watu wote kuwa, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kitaendelea kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazoongoza utendaji wa asasi za kiraia katika kutetea na kulinda haki za binadamu hapa nchini Tanzania.

# Daktari: Nilimpokea Mawazo akiwa taabani

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imeendelea kusikiliza mashahidi wawili katika kesi ya mauaji ya aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Geita, Alphonce Mawazo, inayowakabili washtakiwa watano.

Kesi hiyo namba 9/2019 inasikilizwa na Naibu Msajili Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza ambaye ni Hakimu Mkazi Mwandamizi mwenye Mamlaka ya Ziada (Extended Jurisdiction), Frank Mahimbali, na mashahidi wawili wa Jamhuri walitoa ushahidi juzi jioni.

Washtakiwa hao ni Alfan Apolinari (41), Epafula Zacharia (39), Hashimu Sharifu (45), Habibu Feruzi (34) na Kululinda Bwire (31) wote kwa pamoja ni wakazi wa Katoro mkoani Geita.

Shahidi wa pili upande wa Jamhuri, Daktari Mfawidhi mstaafu wa Kituo cha Afya Katoro, Daniel John (52), akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Javelin Rugaihuruza, alidai Novemba 14 mwaka 2015, alikuwa kwenye shughuli zake za kuwahudumia wagonjwa majira ya saa 7 mchana wakati anawahudumia wagonjwa alisikia kelele na alitoka nje ili kujua kuna nini. Baada ya kutoka nje aliona kuna watu wamemleta mgonjwa ambaye alikuwa akivuja damu kichwani na hali yake ilikuwa mbaya.

"Alidai alinitambua mimi kama daktari na naomba unisaidie, mimi nilimpokea akiwa na PF3 akiwa na askari polisi Mashaka Mahira ambaye ni Mkuu wa Upelelezi wa Kituo cha Polisi Katoro," alidai na kuongeza:

"Hapo hospitali kulikuwa na watu wengi sana na sura zao zilikuwa na hasira, na walikuwa wakisema mtu huyo amepigwa na alikuwa akiitwa Alphonce Mawazo."

Shahidi aliendelea kueleza kuwa alimchukua Mawazo na kumpeleka wodini, huku akiwa na jeraha kichwani, kisogoni na katikati ya kichwa.

Daktari huyo alidai Mawazo alishonwa nyuzi 8 kichwani, jeraha la karibu na kisogo alishona nyuzi 14 na jeraha jingine lilikuwa karibu na sikio alishona nyuzi 2.

Alisema baada ya kumaliza kushona majeraha, hali ya Mawazo iliendelea kuwa mbaya huku damu ziliendelea kuvuja, ndipo alimwandikia rufani kwenda Hospitali ya Wilaya Geita.

Shahidi wa tatu wa Jamhuri, Elizabert Paskari (48) mkazi wa Katoro Mkoa wa Geita akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Javelin Rugaihuruza, alidai Novemba 14 mwaka 2015 majira ya asubuhi CHADEMA walikuwa na kikao kwenye ukumbi wa Makungu mtaa wa eneo la CCM Katoro ambacho kiliitishwa na Mawazo kwa ajili ya kuwachagua mawakala ambao wangesimamia uchaguzi wa udiwani ambao ulikuwa umeahirishwa Kata ya Rudete.

Alidai wakati mkutano huo unaendelea mmoja wa wajumbe, Jackson alitoka nje kujisaidia na aliporejea ndani akasema kuna mtu nje anawarekodi mazungumzo yao.

Shahidi huyo alidai baada ya taarifa hizo watu kwenye ukumbi walitaharuki na kutoka kwenye ukumbi, na kwamba vijana walimshika na kumuuliza kuwa yeye ni nani mpaka awarekodi mazungumzo yao.

"Huyo mtu alijibu kuwa yeye ni usalama wa Taifa, ndipo Mawazo akawaambia vijana msimpige kwa sababu huu ni mtego...mkimpiga mtaniletea matatizo, kwa kuwa yametokea hayo ondokeni na hali itakapokuwa shwali tutajulishana na tutaendelea na kikao chetu.

Alidai baada ya kutoa taarifa hiyo, Mawazo aliita pikipiki ili aende Geita Mjini, na kuahidi hadi hali itakapokuwa swali atarudi.

Shahidi alidai wakati wanashangaa ukumbini zilifika magari mawili yalifika eneo la ukumbi wakateremka watu wakiwa wamevalia sare za CCM wakiwa na marungu, mashoka na fimbo wakaelekea ukumbini walipokuwa wanachama wa CHADEMA.

Alidai watu hao walikuwa 10 hadi 15 wakati huo ilikuwa ni majira ya saa 5 asubuhi, na aliwatambua wengi kwa sura na wengine kwa majina yao. Aliodai kuwatambua ni Alfan Apolinari, Epafula Zacharia na Hashimu Sharifu.

Aidha, alidai mshtakiwa Alfani Apolinari alikuwa anamfahamu tangu mwaka 2009 baada ya kuingia CHADEMA kwa sababu walikuwa wakigongana mitaani kutafuta kura.

Pia alidai Alfan alikuwa akiishi Katoro na alikuwa akijihusisha na uchimbaji wa madini, na wakati akishuka kwenye gari eneo la ukumbini alikuwa amebeba moko ya kuchimbia dhahabu.

Pia alidai mshtakiwa Epafula Zacharia anamfahamu kama mfanyabiashara wa baskeli tangu mwaka 2012, na kuwa aliposhuka kwenye gari eneo la ukumbini alikuwa amebeba panga na mshtakiwa Hashimu Sharifu anamfahamu kama mchezaji wa timu ya mpira Katoro Star, na aliposhuka kwenye gari alikuwa amebeba fimbo.

Alidai baada ya kushuka kwenye gari walisema 'baba yenu yuko wapi, leo siku zake zimeisha, baada ya Mwenyekiti Alphonce Mawazo kutoka hapo ukumbini, washtakiwa hao walielekea njia ambayo Mawazo alipita.

Alidai: "Washtakiwa walielekea Mawazo alipoelekea, na wengine waliondoka kwa miguu, wengine kwa gari na wengine wakanirudia mimi na kuanza kunishambulia wakiwa wamevalia sare za CCM."

"Mshtakiwa wa tano ambaye nilimtambua kwa sura ndiye aliyenikata na panga kichwani, na kijana mmoja aliyejulikana kwa jina moja la Bahati ndiye aliyenisaidia kwa kuwatupia jiwe wafuasi wa CCM wakaniacha mimi wakamkimbiza Bahati na mimi nikaondoka kwenda kituo cha polisi Katoro,"

"Nilipofika kituoni hapo sikupewa msaada wowote bali nilifukuzwa na kuambiwa kuwa toka hapa siwezi kuwasaidia nyinyi watu wa CHADEMA mpaka tupate maagizo kutoka kwa mkuu wa kituo, mimi nikaondoka."

Alidai baada ya kuondoka kituoni, alipigiwa simu na kiongozi wake wa chama, aliyemtaja kwa jina la Charles akimwambia ameshaondoka na mmoja wa askari kuwa amekubali nirudi kituoni.

Baada ya kufika kituoni wakati askari Stella anamwandikia PF3, Charles alimwambia kuwa aendelee, lakini wao wameenda kwa Mawazo kwa kuwa amejeruhiwa vibaya na yuko Kituo cha Afya Katoro.

Kesi hiyo itaendelea leo kwa upande wa Jamhuri kuendelea kutoa ushahidi.



Washtakiwa Alfan Apolinari (41), Epafula Zacharia (39), Hashimu Sharifu (45), Habibu Feruzi (34) na Kululinda Bwire (31), wakazi wa Katoro Mkoani Geita, wakiwa chini ya ulinzi mkali wa polisi juzi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita. **PICHA: JOCTAN NGELLY**


**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**COMMERCIAL CASE NO. 80 OF 2020**

**SAO HILL INDUSTRIES LIMITED......................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**NIPO GROUP LIMITED......................DEFENDANT**

**SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION**

**TO:**
**MANAGING DIRECTOR,**
**NIPO GROUP LIMITED,**
**PLOT NO. 43, BLOCK M,**
**KISASA NORTH,**
**P.O.BOX 1109, DODOMA**

**TAKE NOTICE** that the plaintiff has instituted a suit against you with particulars set out in the plaint filed in this court. Service of the summons on you has been ordered by means of this publication.

You are directed to collect copies of the summons and plaint from the Court's Registry, P.O.Box 12533, Dar es salaam. You are ordered to file your written statement of defence within twenty one (21) days of publication of this notice. You are hereby summoned to appear in this Court in person or by an Advocate or an agent duly authorized on 24th day of February, 2021 at 11:00 am when this case will be heard.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** should you default to file your written statement of defence and/or enter appearance as herein provided, the suit will proceed and a decision may be given in your absence.

Given under my hand and the seal of the Court this 3rd day of December, 2020.

DEPUTY REGISTRAR



Spika wa Bunge mstaafu, Anna Makinda, akizungumza na washiriki wa maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, yaliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Mabibo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# Wito watolewa kupima macho kila mara

**Na Enock Charles**

WATANZANIA wametakiwa kutunza macho yao kwa kufanya upimaji ili kubaini kasoro mbalimbali zinazoweza kujitokeza kuepuka upofu unaoweza kuepukika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Standard Chartered, Sanjay Rughani, akizungumza katika kukamilisha programu ya 'Kuona ni kuamini' mkoani Singida inayolenga kutokomeza upofu kwa kushirikiana na Sightsavers, alisema ni muhimu kuimarishwa kwa mifumo ya afya nchini ikiwamo kuanagalia suala la macho.

"Ripoti ya dunia juu ya afya ya macho inaonyesha kwamba ulimwenguni zaidi ya watu bilioni 2.2 wana shida ya kuona kati ya hao watu angalau bilioni 1 wana shida ya kuona, ambayo ingeweza kuzuiwa au bado haijatibiwa, hivyo kupima macho na utunzaji ni jambo muhimu," alisema Rughani.

Mradi huo uliogharimu dola milioni 1.5 kutoka benki hiyo, ulioanza tangu mwaka 2016 ulilenga kuchangia utoaji endelevu wa huduma za utunzaji wa macho, kuimarisha mifumo ya afya ya macho, kutoa huduma bora za afya ya macho, kuongeza upatikanaji wa huduma za afya ya macho katika wilaya zote za Singida na kuongeza msaada na kujitolea kwa afya ya macho kutoka serikali za mitaa na serikali kuu.

Mradi huo ulifikia shule 483 kati ya 529 ambazo ni sawa na asilimia 91 ya jumla ya shule za msingi mkoani Singida, huku jumla ya wanafunzi 203,248 wakichunguzwa na kati yao wanafunzi 10,665 walipewa miwani na wanafunzi 8,465 walitibiwa kwa matatizo tofauti ya afya ya macho. Mbali na watoto, watu wazima katika mkoa wa Singida pia walinufaika na mradi

huo ambapo watu wazima 106, 990 walipimwa na 8,638 walifanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho wakati 6,154 walipokea miwani huku 81,366 wakipokea matibabu ya afya ya macho.

Mradi huo pia ulihusu ujenzi wa huduma ya macho na vituo vya afya, ambapo ulisaidia ujenzi wa kliniki tano za afya ya macho katika wilaya za Manyoni, Iramba, Singida, Ikungi na Mkalama, ambazo zimejengwa kwa kushirikiana na serikali.

Rughani alisema ushirikiano wa karibu na serikali katika utekelezaji wa mpango wa kuona ni kuamini utasaidia sana kuhakikisha uendelevu wa programu hiyo muhimu kwa mustakabali wa afya ya macho kwa wananchi.

"Wakati mradi wa 'Kuona ni Kuamini' umefikia tamati, ninafurahi kujua kwamba kuna mpango endelevu wa kuhakikisha juhudi zaidi zinaelekezwa katika kutokomeza upofu unaoweza kuepukika," Rughani alisema.

Naye Mkurugenzi wa Sightsavers nchini, Godwin Kabalika, aliipongeza Benki kwa kufadhili mpango wa Kuona ni Kuamini ambao umebadilisha maisha ya watu wengi huko Singida na Tanzania kwa ujumla.

# Wadau mafuta ya kula wapewa mafunzo

**Na Mwandishi Wetu,**
KIGOMA

ZAIDI ya wakulima, wasindikaji, wasambazaji na wauzaji wa mafuta ya kula hususani mawese 12,200 mkoani Kigoma, wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji, usindikaji na utunzaji wa mafuta kwa kuzingatia matakwa ya viwango na vifungashio bora ili kuongeza thamani ya mafuta hayo.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Lazaro Msasalaga, alisema ili mafuta ya kula yawe bora ni lazima kuzingatia kanuni bora za kilimo, usindikaji na afya.

Msasalaga alisema wazalishaji wengi wa mawese na mafuta mengine ya kula wamekuwa wanatumia njia za asili ambazo hazizingatii ubora na usalama wa mafuta hayo na hivyo kusababisha madhara kwa walaji.

Kaimu Mkuu wa TBS Kanda ya Magharibi Rodney Alananga, aliwataka wasindikaji kufuata taratibu za uthibitishaji ubora wa mafuta hayo kwa kuwa kwa kufanya hivyo kutaongeza masoko ya ndani na nje ya nchi na kulinda afya na usalama wa walaji.

Naye Meneja Mafunzo na Utafiti wa TBS, Hamis Sudi, akifunga mafunzo hayo katika Kata ya Ngaruka, alisema serikali inathamini mchango wa wajasiriamali katika kukuza uchumi wa nchi.

Sudi alisema mbali na mafunzo hayo, TBS imekuwa ikitoa huduma za kuthibitisha ubora wa bidhaa za wajasiriamali bure kwa miaka mitatu ya kwanza kuwawezesha wajasiriamali kukua na kuzalisha bidhaa bora ambazo zitashindana katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

"Ninawasihi wajasiriamali mtumie fursa hii muhimu ambayo serikali imewapatia ili muweze kuinua kipato chenu binafsi na taifa kwa ujumla," alisisitiza Sudi.

Ofisa Biashara kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, Festo Kapela, alisema zaidi ya asilimia 50 ya mafuta ya kula yanayotumika nchini hutoka nje ya nchi kwa kutumia gharama kubwa na kwamba ikiwa mafuta ya mawese yatapewa ubora, serikali itaokoa gharama kubwa.

"Nchi za Afrika Mashariki na kati zinategemea sana mafuta ya nje ya nchi. Kama viwanda vya kuchakata mafuta ya mawese vitaongeza ubora, itakuwa fursa kwa wakulima na wasindikaji kuongeza pato la taifa kupitia soko la mafuta," alisema Kapela.

# Upanuzi kituo afya kukamilika mwisho wa mwezi

**Na Sabato Kasika**

UPANUZI wa Kituo cha Afya cha Kata ya Bugwema, Wilaya ya Musoma mkoani Mara ulioanza mwanzoni mwa mwaka huu, unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu.

Katika kufanikisha upanuzi huo, serikali imetoa Sh. milioni 400, huku wananchi nao wakichangia nguvukazi zao ikiwamo kusomba mawe, maji, mchanga, kokoto pamoja na fedha taslimu.

Akizungumza na gazeti hili, Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, alisema kazi ya ujenzi inaendelea vizuri, na kwamba kuna uwezekano wa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu.

"Serikali imetoka Sh. milioni 400 na wataalamu mbalimbali ikiwa ni mchango wake kwa mradi huu wa upanuzi wa zahanati kuwa kituo cha afya, na wananchi nao wanachangia nguvukazi," alisema Dk. Anney.

Alifafanua kuwa kituo hicho kitakapokamilika na kuanza kutoa huduma za afya, kitakuwa ni cha tatu katika Wilaya ya Musoma yenye halmashauri mbili, vikiwamo vya Murangi na Mugango ambavyo vinafanya kazi.

"Tunaendelea kuwaomba wadau watuunge mkono, ili kuboresha huduma za afya, ambacho kitakuwa na huduma za maabara, X-ray, chumba cha kuhifadhia maiti, wodi ta mama na mtoto na sehemu ya kufulia," alisema.

Naye Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, alisema, ahadi yake katika upanuzi wa zahanati kuwa kituo cha afya ni mifuko 400 ya saruji, ambayo tayari ameanza kutoa.

"Si katika afya tu, bali nimekuwa nikichangia maendeleo ya jimbo langu kwenye sekta mbalimbali ikiwamo elimu na kilimo pia, kwa kushirikiana na wananchi ili kuboresha huduma hizo jimboni," Prof. Muhongo alisema.

Diwani wa Kata ya Bugwema, Cliford Musiba, alisema, aliahidi kusomba maji ya ujenzi kwa kutumia gari lake, na kwamba lilitumika kwa muda wa miezi minne na kukamilisha kile alichokuwa ameahidi.

"Yaani ni kwamba, usombaji wa maji ya ujenzi kwa gari la kukodi ilikuwa ni Sh. 300,000 kwa siku, hivyo nikaone gari langu litumike kufanya kazi hiyo bure kwa muda wa miezi minne," alisema Musiba.

Alisema, Kata ya Bugwema inaundwa na vijiji vinne alivyovitaja kwa majina ya Bugwema yenyewe, Masinono, Muhoji na Kinyang'erere, na kwamba ina jumla ya wakazi 14,029.

# Akaunti sasa kufunguliwa Stanbic bila kwenda tawini

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya Stanbic Tanzania imeendelea kuleta mapinduzi ya kidigitali, baada kuzindua huduma ya kibenki ambayo inamwezesha Mtanzania yoyote kufungua akaunti yake mwenyewe bila kwenda kwenye tawi.

Huduma hiyo iitwayo 'Bofya Bofya' inalenga kuboresha huduma za ufunguaji wa akaunti nchini na kufanya ziwe fasaha na rahisi. Wateja watatakiwa kuingia katika tovuti ya benki na kufungua akaunti zao moja kwa moja.

Benki hiyo imeeleza kuwa huduma hii ni salama na inalindwa na uthibiti wa njia mbili kutumia SMS.

Akizungumzia huduma hiyo, Mkuu wa Kitengo cha huduma za matawi na kidigitali wa benki Stanbic, Jennifer Hillal, alisema: "Kutokana na ukuaji wa kasi katika sekta ya malipo kwa njia ya elektroniki, wateja wetu wanazaidi kutafuta njia za haraka, salama na zenye unafuu kutumia katika malipo. Ndio manaa tumewaletea huduma ya Bofya Bofya ili kila Mtanzania aweze kufungua akaunti popote alipo na kwa urahisi."

Naye Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Ruth Mwaiselage, alisema: "Huduma ya Bofya Bofya ni ya watu wote, hasa waliopo maeneo ambayo ni ngumu kwenda kwenye matawi.

Mteja atatakiwa kuwa na kitambulisho cha taifa tu ili kufungua kaunti na hakutakuwa na gharama yoyote, hata kianzio."

Aliongeza kuwa Stanbic siku zote inalenga kuwa mstari wa mbele katika kuleta huduma bunifu, ili kuboresha utoaji huduma kwa wateja wao na kuhakikisha huduma za kibenki zinawafikia watu wengi nchini.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo (wa pili kulia), akikata utepe kuzindua duka jipya la kisasa la Vodacom katika Barabara ya Haile Selassie, Masaki jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Stella Msofe (wa pili kushoto), Mkuu wa Mauzo wa Vodacom Kanda ya Dar es Salaam na Pwani, Brigita Stephen (kulia) na msimamizi wa duka hilo, Emmanuel Makaki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamati zaanzishwa kupambana na ukatili

**Na Yasmine Protace**

KATIKA kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia, serikali imeanzisha kamati 16,313 ambazo zipo kila kona kwa ajili ya kupambana na matukio ya ukatili.

Hayo yalisemwa na Dalius Demasi, Ofisa Ustawi wa Jamii Mkuu kutoka Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

Demasi ambaye alishiriki maadhimisho hayo yaliyofanyika katika viwanja vya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), alisema kuwa kuanzishwa kwa kamati hizo kila kona ni mikakati ya kupambana na matukio ya ukatili.

"Katika kupambana na matukio ya ukatili, serikali imeanzisha kamati 16,313 katika kila kona, ili kupambana na matukio ya ukatili," alisema.

Aliongeza serikali imetekeleza mpango wa kupambana na matukio ya ukatili, na kwamba mpango huo upo katika Ilani ya uchaguzi ya CCM.

Alisema serikali imefanya jitihada mbalimbali kwa kuanzisha mafunzo ya kuwalinda wanawake na watoto dhidi ya matukio ya ukatili.

Aliongeza kuwa katika kupambana na matukio ya ukatili, madawati ya kusikiliza matukio hayo yameanzishwa, magereza, polisi na vyuo vikuu mbalimbali lengo ni kupinga ukatili wa kijinsia.

"Mbali na kuanzishwa kwa madawati, magereza, polisi na vyuo, pia wameanzisha madawati katika baadhi ya shule ili wanafunzi wawe wanatoa taarifa pale wanapofanyiwa ukatili wa kijinsia," alisema.

Anna Malinda ambaye alikuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo ya siku 16 za kupinga ukatili, alisema kutokomeza ukatili inatakiwa kuwapo na nguvu ya amoja.

# Wazalishaji mabomba ya plastiki waiangukia serikali

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZALISHAJI wa mabomba ya plastiki nchini wameiomba serikali kudhibiti uingizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje, kwamba itasaidia kuinua viwanda vya ndani.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Mwendeshaji Mkuu wa Kampuni ya uzalishaji mabomba ya plastiki (PLASCO Ltd), Alimiya Osman, wakati akizungumza na waandishi wa habari, kueleza kwamba uingizaji wa bidhaa za plastiki kutoka nje kunaua viwanda vya ndani.

"Tatizo kubwa linalotukabili sisi wazalishaji wazawa ni uingizaji wa bidhaa kutoka nje, bidhaa hizo zikishaingia nchini zinauzwa kwa bei ndogo kwa sababu zinakuwa hazijalipiwa ushuru huko zilipotoka," alisema Osman.

Osman alisema tatizo lingine ni kukatika kwa umeme mara kwa mara, hali inayosababisha kuharibika kwa bidhaa pamoja na kusimama kwa uzalishaji, pamoja na uwapo wa bidhaa feki.

Alisema PLASCO Ltd imeanzisha teknolojia iitwayo Weholite iliyogharimu Dola za Marekani milioni sita (Sh. bilioni 13.838), ambayo inatumika katika utengenezaji wa mabomba imara ya kupitisha maji, ujenzi wa makalavati, pamoja na mfumo wa umwagiliaji katika kilimo.

Osman alisema serikali ya awamu ya tano imefanikiwa kwa asilimia kubwa kutatua matatizo yanayowakabili wazalishaji wazawa, kupitia Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI).

Alisema: "Tunajisikia furaha kuona serikali ikidhibiti uingizaji wa bidhaa za mabomba ya plastiki, awali ilikuwa ni vigumu kwetu kushindana katika masoko."

Alisema PLACO Ltd ilianzishwa mwaka 1993 na imekuwa ikisambaza bidhaa katika nchi za Rwanda, Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kwamba mbali na uzalishaji wa mabomba kwa ajili ya mafuriko, pia wanazalisha mabomba kwa matumizi ya gesi, umwagiliaji, pamoja na miradi ya maji.

Aliongeza: "Lengo letu ni kuwaridhisha wateja, bidhaa zetu ni bora na vimethibitishwa na maabara za kimataifa."

Naye, Mhandisi na Mtaalam wa mauzo wa Kampuni ya PLASCO Ltd, Mafikri Mushi. alisema wanazalisha mabomba ambayo ni bora katika upitishaji wa maji wakati wa ujenzi wa barabara.

Alisema: "Tunaiomba serikali na wadau kutumia mabomba ya PLASCO Ltd katika kudhibiti mafuriko katika sehemu mbalimbali za Jiji la Dar es Salaam."



Ukurasa 12

**Halmashauri ya Tarime yawekeza kituo afya cha kisasa, kilio chake wataalamu**




Ukurasa 14

**Vita kukabili corona vimeshamiri, kufikia wengi ng'ambo ya Afrika, ni kitendawili**

# Tafsiri mpya ya Msalaba Mwekundu itakavyohudumia afya miaka 5 ijayo

**Na Yasmine Protace**

CHAMA cha Msalaba Mwekundu nchini, kimeandaa mkakati wa miaka mitano ijayo, ikija na mabadiliko makubwa katika utoaji wa huduma zake katika sekta ya afya.

Mabadiliko yanajumuisha programu mahsusi za kusaidia maeneo mtambuka, wakiwamo watoto yatima na wagonjwa wa Ukimwi, tamko lililowasilishwa rasmi na rais wa chama hicho, David Kihenzi.

Ni mkutano uliowashirikisha wajumbe na wenyeviti kutoka mikoa ya Tanzania Bara na Visiwani, maelekezo yakiwashukia watenda kazi, wawakilishi wa vijana na watumishi wote wa chama hicho.

Kihenzi ambaye ni Mbunge wa Mufindi, anasema taasisi imejipanga kuendeleza kufanya mabadiliko makubwa ya kiutendaji katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Anaainisha mikakati ya miaka mitano, inagusa kuwa na programu ya kuwasaidia yatima, wakiwamo wagonjwa wa Ukimwi.

“Tutawasaidia watoto wawe na maisha bora. Tutawasaidia wajiendeleze pale watakaposhindwa wajiajiri baada ya kupatiwa mafunzo ya ufundi seremala,” anaeleza Kihenzi.



Baadhi ya wenyeviti na watumishi wa Msalaba Mwekundu, nchini wakiwa pamoja. **PICHA: YASMINE PROTACE**.

Ulikuwa ufafanuzi wa kimkakati, anaoutaja ni kujikita katika maendeleo ya kiofisi, yanayoitaka taasisi iwe na matawi imara na watu wa kujitolea, wenye weledi unaostahili.

Mkakati mwingine anautaja, ni namna ya kuhakikisha matawi yanakuwa chachu katika changamoto za kijamii, sambamba na kuwa na viongozi waelewa wa majukumu yao, ikiwamo kusimamia shughuli za kitaasisi katika maeneo yao.

Anasema, kuna mkakati wa maendeleo ya kitaasisi ambayo ni kuwahamasisha wananchi wapate wanachama wanaoongeza nguvu za vijana na anafafanua: “Vijana wana malengo makubwa kutokana na kuwa na ubunifu.”

Pia, anataja haja ya kuwapo matawi na ofisi na vikosi kazi katika kufanya kazi katika maafa, akiwa na ufafanuzi wa mkakati mwingine wa kuongeza programu mbalimbali, wakiwa wamejipanga kuendeleza masuala ya afya.

Kuhusu idadi ya wanachama, anasema katika kipindi cha mwaka jana, kulikuwapo na wanachama 20,000 ambao kuanzia Januari mwaka huu kuna wanachama 58,000, na wapo vijana wa kujitolea 100,000 wanaodhamiria kuwaongeza, kufanyike kazi kubwa zaidi.

Katibu wa Chama cha Msalaba Mwekundu, Julius Kejo, anataja mikakati mingine, ni namna wanaamua kuwa na vikosi kazi katika kukabili maafa katika kila ofisi nchini.

Anaeleza, azma ya kuendeleza program mbalimbali, kama za kuendeleza shughuli za afya, kuwasaidia watoto yatima walioshindwa kwenda shule, ili wafanikishwe kujiajiri wakiwa na stadi za ufundi seremala.

Pia, ndani ya mkakati huo, familia zinazoishi na watoto wenye shida watasaidiwa na kuna ufafanuzi:

**HUDUMA SAFI**

“Kuna jamii ambazo hazina majisafi na salama, hivyo watasaidiana na serikali kuhakikisha watu wanakunywa majisafi na salama,” anasema.

Chama cha Msalaba Mwekundu, pia kinasogea kuwezesha jamii kupata huduma ya vyoo safi na salama, ikianzia na namna ya kuelimisha jamii kupunguzoa majanga ya kiafya.

Katibu Mkuu wa Msalaba Mwekundu, anaeleza dhamira nyigine za utekezaji mkakati wao, kwa wasiojiweza na walemavu ambao hawakuwahi kuwafikia.

Kejo anarejea sheria inayoipa Chama cha Msalaba Mwekundu jukumu la kuwajibikia majanga pindi yanapotokea.

Rai yake ni jamii inapaswa kujiandaa kutoa taarifa sahihi na mapema, pale wanapobashiri shida na hiyo inafanyika kupitia jamii kujikinga na athari zinazoweza kujitokeza, ili wachukuwe hatua stahiki.

Kejo anasema hivi sasa wanajiandaa kununua vifaa vya kukabiliana vitakavyowaokoa na tayari Msalaba Mwekundu umeshajenga ghala mkoani Dodoma, kunakohifadhiwa vifaa stahiki, kupeleka mahali husika inapotokea.

Anasema wana mfumo wa ushirikishaji jamii, pale panapotokea tatizo, wairudishie jamii katika hali zao za kawaida.

“Yote hayo yanafanywa kwa ajili ya kulenga familia zilizo na hali ya chini kabisa,” anasema Kejo, akiutaja

mkakati mwingine ni kuwa na mfumo bora wa fedha na rasilimali fedha, zinazotumika katika shughuli zilizolengwa.

**TEHAMA**

Anautaja mpango mkakati walio nao sasa, ni kuboresha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (T EHAMA), kwa manufaa ya kuibua taarifa ya vyote vinavyotokea, zaidi ikilenga miradi mikuu ya jamii ya wakimbizi, anakokutaja walioko Kigoma, Kakonko na Kibondo, sehemun kuu ya majukumu ni kulaza wagonjwa na wanaofika kutibiwa na kuondoka.

Kejo anafafanua kinachofanyika hapo ni kuhudumia wajawazito chakula cha jumla, wagonjwa wenye mahitaji maalum, maji na hata uchangiaji damu.

AFYA

# Halmashauri ya Tarime yawekeza kituo afya cha kisasa, kilio chake wataalamu

## • DED: Tuliguswa kuwapunguzia wagonjwa safari

**Na Anthony Gervas, aliyekuwa TARIME**

KATIKA Mpango wa Maendeleo ya Afya (MMAM) ulioanza mwaka 2008, lengo lilizama katika maeneo makuu matano; zahanati kwa kijiji na mitaa, kata za vituo vya afya, wilaya, inakuwa na hospitali, huku mkoani kunakuwapo hospitali ya rufani.

Juu ya mkoa kuna hospitali za kanda mbalimbali nchini na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Wakati hatua kubwa imeshapigwa kwa mafanikio kamili, bado kuna juhudi zinazoendelea kufikia malengo hayo, kama vile katika takwimu za hatua zinazotolewa na serikali kila mara.

Ndani ya Kata ya Nkende wilayani Tarime, mkoani Mara, watu wamekuwa wakitaabika kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma za kina katika Hospitali ya Wilaya ya Tarime, inayoelemewa na wagonjwa.

Hapo ndipo hatua ilichukuliwa na Mganga Mfawidhi wa Hospitali Wilaya ya Tarime, Dk. Innocent Kweka, anayefafanua "(Magena) ilikuwa zahanati, lakini tukaona tuipandishe hadhi hadi kituo cha afya.

"Lengo ni kupanua huduma za afya katika kata ya Nkende na kuwaondolea kero wananchi ya kutembea umbali mrefu hadi katika Hospitali ya Wilaya na mrundikano wa wagonjwa uliokuwapo."

Dk. Kweka anadokeza kasoro inayoendelea sasa ni katika ngazi ya wilaya kuna upungufu wa wauguzi 80 kati ya 200 wanaohitajiwa.

Pia, wakati katika Kituo cha Afya Nkende kuna waganga 10 kati ya 20 wanaohitajika, Ofisa Tabibu wa kituo hicho Emmanuel Masunga, ana ufafanuzi kuwa:

"Hivi sasa mtaalamu wa maabara yupo mmoja tu na wauguzi wapo saba, lakini ili kutosheleza huduma wanahitajika wataalamu wa maabara watatu na wauguzi jumla yao 12."

Masunga anaongeza kuwa, hadi sasa kituo hicho kipya cha afya hakina madaktari bingwa, licha ya kuwapo vifaa vya kazi vinavyotosheleza mahitaji.

Upanuzi kufikia kituo hicho cha afya ulianza mwaka 2018, ukilenga utoaji huduma bora za na kuondoa kero zilizowakabili wananchi, hata baadhi walilazimika kutembea umbali mrefu kufuata Hospitali ya Wilaya ya Tarime.

Baada ya kukamilika na kupanda hadhi kuwa kituo cha afya, tayari inaelezwa panatolewa huduma za upasuaji wajawazito, wodi ya wazazi, maabara na chumba cha kuhifadhi maiti, njia za kupita wagonjwa, sehemu ya kuchoma taka, uzio wa majengo na kuwekwa mfumo wa umeme na maji

Masunga analalamika kwamba upungufu wa wataalamu hasa wauguzi na maabara ambako yuko mmoja, kati ya hitaji la watatu na wauguzi saa kati ya 12, lakini dawa zinapatikana za kutosha.



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Tarime, Innocent Kweka, akiwa ofisini kwake. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS**



Mkurugenzi Mtendaji wa Mji wa Tarime, Elias Ntiruhungwa, ofisini kwake.

### MGANGA WA WILAYA

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya, Dk. Innocent Kweka, anasema pia kuna ujenzi wa nyumba tatu za watumishi, kukarabatiwa wodi na jengo la upasuaji (OPD), huku mpango wa uanzishaji duka la dawa uko mbioni kuwarahishia wagonjwa.

Anasema, wastani ulioko kila mwezi kuna wagonjwa 40 wanaofanyiwa upasuaji, hasa kinamama wanaojifungua kwa huduma za dharura, kidole tumbo(appendix), mishipa ya ngiri na mabusha.

> **"Lengo ni kupanua huduma za afya katika kata ya Nkende na kuwaondolea kero wananchi ya kutembea umbali mrefu hadi katika Hospitali ya Wilaya na mrundikano wa wagonjwa uliokuwapo**

### DED TARIME

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Tarime, Elias Ntiruhungwa, anasema ujenzi wa Kituo cha Afya Magena umegharimu Sh. milioni 568, zikiwamo Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG), jumla Sh. milioni 400.

Anasema, wananchi wamechanga Sh. milioni 9.4 na Halmashauri ya Mji wa Tarime, imechangia Sh.48, 813,882, huku wadau wakiwa ni kampuni.

Ntiruhungwa anasema katika uchangiaji, wadau wa maendeleo mgodi wa North Mara Gold Mine, wamechangia Sh. milioni 110.

Ana ufafanuzi kwamba lengo la kubadilisha hadhi ya zahanati kuwa kituo cha afya, ni kuboresha na kupanua huduma za afya kwa wananchi watakaohitaji matibabu katika kata hiyo na kuwapunguzia safari za mbali.

Mkurugenzi huyo ana ufafanuzi wa manufaa mengine ni kupatikana ajira kwa wenyeji washiriki wa ujenzi.



Kituo cha Afya cha Magena, katika Halmashauri ya Mji wa Tarime, kilichopandishwa hadhi kutoka zahanati.

MAZINGIRA

## MRADI WA FORVAC NYASA...

# Mafanikio ya shamba lenye miti maelfu yanavyokwamishwa na mafuriko mtoni

- Wamiliki msitu walia kujengewa daraja
- Mnyororo thamani unaozaa 'mamilioni'

**Na Christina Haule, NYASA**

MTU anapofika katika kijiji cha Liuli wilayani Nyasa, basi ana nafasi kubwa ya ushuhuda wa thamani wa kimazingira, shamba na misitu ekari 180 chini ya usimamizi wa Programu ya Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC) , ikiwa na jumla ya mitiki 300,000 iliyopandwa na wanavijiji waliohamasika.

Mwenyekiti wa Muungano wa Chama cha Wakulima wa Miti Liuli (TGA) Samuel Mawanja, anasema katika msimu wa mwaka 2019/20 jumla ya wakulima 80 walishanufaika kwa kupanda miti hiyo kutoka kwenye mradi.

Anasema, katika uhalisia huo, mbali kuwa na mamia ya miche ya miti yao, bado wanahitaji idadi ya miche kutoka FORVAC waliopanda, kwa manufaa ya msimu uliopo wa kilimo.

Mawanja anasema, wanalenga kuipanda katika maeneo yao ya vijiji anavyovitaja vya vya Liuli, Nkalachi, Mkali A na B na Lipingo ili kutimiza malengo yao ya ulinzi wa misitu na uhifadhi wa mazingira.

Anasema wamekuwa wakitumia miti iliyopo katika shughuli mbalimbali ikiwamo kutengeneza bidhaa mbalimbali kama vile madirisha, milango na samani za ndani, lakini miti hiyo itakuwa mbadala na kuwafanya kutokata tena miti ya kwenye misitu ya vijiji na kuleta uharibifu.

Mawanja anasema, kwa kiasi kikubwa wanategemea kupata miti hiyo ikiwa bora na kuongeza kutengeneza bidhaa za kuuza na kutumia kama vile mitumbwi mbali na kupata kipato cha kutosha na kuweza kujikimu kimaisha.

Pia, Mawanja hafichi shukurani zake kwa serikali wilayani humo kuwaelimisha wananchi umuhimu wa mradi, kwamba ni mali yao na wakikundi mwishowe kila mmloja atamiliki wastani wa ekari mbili za miti, zinazokuwa na sura ya manufaa kwao mmoja mmoja.



Mratibu wa FORVAC Taifa, Emmanuel Msoffe, akielezea faida za miti ya misaji kwa jamii. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE**



Mratibu wa FORVAC Kongani ya Ruvuma, Marcel Mutunda, akionyesha miche ya miti ya misaji ikiwa kwenye kitalu kwenye shamba la bustani ya Kipiki, Namtumbo, inayotarajiwa kupandwa wilayani Nyasa, mkoani Ruvuma.

**BOSS FORVAC MKOA**

Mratibu wa FORVAC, Kongani ya Mkoa Ruvuma, Marcel Mutunda, anarejea mpango kimkoa kwamba waliamua upandaji miche ya miti katika bustani ya Kipiki kwenye shamba la miti Kwa Mpepo wilayani Namtumbo, katika kivuli kile cha msingi wa mnyororo wa thamani.

Anaeleza muuganiko uliopo, mnyororo wa thamani kuanzia kwenye mbegu, kisha miche na baadaye miti na mwaka 2020/21, wanatarajia kugawa bure miti yenye thamani ya shilingi milioni 300, katika vijiji vinne.

Ni zao litakalobuniwa na wananchi kupunguza uharibifu wa misitu unaonekana kuongezeka katika maeneo wanayoyahisi au kugundua hayana Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii (USMJ).

Anasema mwaka jana wa kilimo, 2019/20 waligawa miche 150,000 yenye thamani ya shilingi milioni 75 kwa wanavijiji hivyo.

Mratibu wa FORVAC Taifa, Emmanuel Msoffe, katika hilo anawaagiza wananchi Nyasa, wahamasishane kuhifadhi safu ya Milima Livingstone, sambamba na kupunguza shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya milima, ili kuhifadhi vyanzo vya maji kwa ajili ya maendeleo endelevu.

Anasema, upandaji miche ya miti inaweza kuendelea hata mradi wa FORVAC utakapoisha mwaka 2022 na wakati huohuo akihimiza miradi mingine ya kuingiza kipato, wakati wanavikundi wa upandaji miti wakisubiri uvunaji miti ya misaji baada ya miaka 20 hadi 25 ijayo.

"Mazao ya muda mfupi wa miezi mitatu kama vile mananasi, parachichi, mihogo, mizinga ya nyuki, inaweza kuwasaidia kupata chakula na fedha kiasi za kujikimu kwa mahitaji ya elimu, chakula na matibabu," anasema Msoffe.

Pia, anasema miti hiyo aina ya misaji, inafaa kutengeneza samani, kuweka sakafu, kutengeneza deki za meli na majahazi na inatumika kama nishati ya kupikia, huku ikiwa mbadala wa ukataji kama mininga, mikongo na mivule.

Msoffe anaipa misaji sifa ya kukomboa maisha ya wakulima katika siku zijazo, pia mradi ni fursa nzuri ya kukuza ujuzi na utaalamu wa kukuza, kupanda na kusimamia miti, jambo ambalo ni ishara ya upandaji wake endelevu.

Wakati ukuaji wa miti hiyo inachukua hadi miaka 20 na 25, katika nchi baridi inafikisha miaka 60, akitaja maeneo yanayostawi nchini ni baadhi yua maeneo ya Tanga, Mtibwa na Kilombero mkoani Morogoro, pia Namtumbo na Nyasa, Ruvuma.

Hadi sasa, Mradi wa FORVAC kitaifa inatekelezwa katika wilaya 12, Kilindi, Handeni, Kiteto, Mpwapwa, Kongani Ruangwa, Liwale, Nachingwea, Tunduru, Namtumbo, Songea, Mbinga na Nyasa.

**KILIO CHA MTO**

Wakati kuna hatua iliyopigwa wilayani Nyasa, Ofisa Maliasili wa wilaya hiyo, Bugingo Bugingo, analalamika mafanikio ya shamba kubwa yanakwazwa na maji yatokanayo na upana wa mto mita 300 hata unafurika haupitiki huku ukimwaga maji kwenye ukanda wa mradi wa miti.

Bugingo ambaye ni Mratibu wa FORVAC Wilayani Nyasa, anashauri FORVAC, serikali na Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) kushirikiana katika ujenzi wa daraja katika mto huo, unaoonyesha kuhitaji kiasi kikubwa cha pesa.

Anasema, daraja hilo likijengwa litasaidia kuondoa shida ya wananchi, ambao anaamini wako tayari kujitolea kusafisha barabara, iwapo daraja wanalilolilia litajengwa kuwaepusha na adha ya kutembea umbali zaidi ya 10 kutoka kilipo kijiji wanakoishi.

Mwanakijiji cha Liuli, Neema Msanso, anaeleza kuwa licha ya kuvutiwa na miliki, upandaji na upaliliaji miti, tabu kuu kwao mto ni mto kujaa maji na wanashindwa kupitika hasa kipindi cha masika, hali inayowalazimisha kulala shambani, kwa kushindwa kurudi majumbani.

"Kuanzia mwezi wa pili, wa tatu, hadi wa nne mto unaotenganisha eneo lilipo shamba na kijiji hujaa na kusababisha wakulima kuwa hawafiki shambani" analalamika.

Mwanakijiji na mwanakikundi cha upandaji miti hiyo, Joseph Ndomondo, anasema daraja litawasaidia kufika na kuondoka shambani kwa wakati na kuwarahisishia kusafirisha mazao ya miti pindi yatakapokuwa tayari kuuzwa, akiamini kuwaongezea zaidi ya biashara pekee ya uvuvi wafanyayo Ziwa Nyasa.

AFYA

# Vita kukabili corona vimeshamiri, kufikia wengi ng'ambo ya Afrika, ni kitendawili

## • Uingereza yajitosa 'mashindanoni' rasmi wiki hii

**Na Nimi Mweta**



Uandaaji dawa ya kinga ya corona, ukiendelea katika Chuo Kikuu cha Oxford, Uingereza. Picha nyingine, dawa ya kinga inayotarajiwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

WIKI hii nchini Uingereza, kunashuhudiwa kuanza kutumia chanjo dhidi ya maradhi yao corona, huku kukitawaliwa na tathmini na ufuatiliaji mkubwa wa kijamii na hata wanasayansi wa ndani na kimataifa.

Ni simulizi yenye mkondo mrefu na msuguano wa hoja za kitaifa kimataifa, ndani yake kukibebwa na harufu ya siasa za msuguano wa wakubwa duniani.

Itakumbukwa, baada ya kampuni ya dawa ya Pfizer, ikishirikiana na BioNTecb, kukamilisha hatua ya tatu ya majaribio ya chanjo ya ugonjwa wa corona, ambazo zilibebwa ishara zimeharakishwa kiasi fulani, Uingereza imekuwa ya kwanza kuruhusu chanjo hiyo ikiwa imekamilika.

Sababu kubwa iliyoko ni shaka kuwa zilizopo mezani zinatoa tarakimu ya uhakika wa kuzuia virusi vya corona na usalama wa matumizi yake katika asilimia 95 na 90.

Hata hivyo, baadhi ya chanjo kama hizo katika nchi za Russia na China, hazikujaribiwa na kupembuliwa katika nchi za magharibi.

Russia ilishaanza kutumia chanjo yake Sputnik V, wakati China ilikuwa inajiandaa, inavyojipanga haitaki kutengwa na soko la nchi za Magharibi.

Kimsingi, chanjo zilizotayarishwa ziliomba kuanza kutumika kwa dharura, kutokana na hali mbaya ya corona katika nchi za Magharibi na maeneo mengi duniani.

Kulikuwapo hitilafu kadhaa wakati wa kufikia majaribio ndani ya hatua tofauti, baada ya ngazi ya kujaribu chanjo tarajiwa kwa wanyama kupitia kinachoitwa 'NQ NQ NQ.'

Chanjo tarajiwa ya kampuni ya AstraZeneca ambayo kimsingi iliundwa katika Chuo Kikuu cha Oxford nchini Uingereza, ilikwama kwa muda mwezi Septemba wakati mtu anayetumika kwa jaribio, alipougua ghafla. Hali hiyo ilionekana kupita kwa haraka na ufafanuzi wake ni kama linawekwa kando.

Mkanganyiko mkubwa upo katika uanzaji kutoa chanjo kwa hatua tofauti za walengwa kwa sasa, inaelekea kwa walio mstari wa mbele kupambana na corona, halafu walio hatarini zaidi, watakaorodheshwa na kupewa chanjo.

Ni aina ya sindano zinazopigwa mara mbili, kwa kipindi cha takriban wiki mbili kabla ya chanjo ya pili, hivyo madaktari na wauguzi ndiyo wanaotangulia, halafu wakazi wa nyumba maalum za kuangalia wazee, ambao ni miongoni mwa waathirika zaidi Marekani na kwingineko.

### HATUA ILIYOFIKIWA

Akitoa taarifa kuhusu mkakati wa kuanza wimbi la chanjo nchini Uingereza, Waziri Mkuu Boris Johnson, aliwaasa wananchi wasianzishe foleni za kutaka chanjo, kwani wanajulikana walipo na wataitwa.

Hadi sasa kuna mijadala inaendelea kuhusu idadi ya watu ambao wanaweza wakakataa chanjo, kwani hilo pia ni suala la hisia na mara nyingine yako mapokeo ya kuwatisha watu kuwa dhamira mbaya imelengwa katika suala hilo.

Watu wa makundi tofauti katika jamii na hasa nchini Marekani, walikuwa wametia shaka, mmoja wao akitamka: "Mimi sitaki chanjo; watu wote (wengine) wakishapata chanjo na mimi nitakuwa salama."

Kuna mtazamo kwamba, haitakuwa jambo la kushangaza kama waliokuwa wanabeza kuvaa barakoa, wabeze kupata chanjo, pia wasiwasi wa kuwapo tofauti, mathalan mwilini, hasa kwa vile hakuna kampuni ambayo hadi sasa imethubutu kusema chanjo hiyo ni salama kwa asilimia 100.

Wakati haitazamiwi kuwa wananchi walio wengi watafikia ngazi ya kupata chanjo huko Marekani na

Uingereza, pia kwingineko kabla ya mwezi Machi au hata Juni mwakani, bado hakuna mjadala wa wazi kuhusu gharama na mipango halisi ya kupatikana chanjo kwa nchi zilizobaki, kama barani Afrika.

Kampuni za Pfizer ya Marekani na BioNTech Ujerumani, chanjo zao zimetangulia kuruhusiwa kutumika na zinahitaji uhifadhi wa kiasi cha nyuzi joto 70, ila kwa siku tano za mwisho inaweza kukaa kwenye jokofu la kawaida, hadi nyuzi sifuri.

Iko wazi Afrika haitalengwa katika mtazamo bado ni mapema sana. Wakati chanjo zinatazamiwa kuwa ndiyo silaha kuu katika kupambana na corona, tiba tofauti zinaendelea kufanyiwa utafiti na matokeo itakuwaje.

Suala la itakuwaje inategemea wagonjwa wanaotumia dawa hizo, kama vile mfano Rais Donald Trump wa Marekani alivyoshangaza wengi, alipopona ndani ya siku tatu.

Pia, bado ni kitendawili cha kupata takwimu za dawa inayofaa zaidi, kwani mara nyingi ni mchanganyiko unaotumika, kwa vile corona inaposhambulia inavunja kinga za mwili na kuwezesha magonjwa yaliyopo kushamiri.

Hivyo, kuna miundo tofauti ya dawa mchanganyiko zinazofaa kutumia kwa wagonjwa wa aina mbalimbali hivi sasa, ingawa juhudi za kufikisha chanjo bora itakayopatikana hazijawekwa pembeni.

### MKURUGENZI WHO

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO), Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus, alitoa wito wa kusambazwa dozi za chanjo kwa usawa unaohitajika pindi itakapopatikana.

Aligusia chanjo tarajiwa ya Pfizer, akiashiria kuwa inatakiwa ipatikane kwa wahitaji na siyo Marekani na nchi kadhaa tajiri zaidi.

Dk. Tedros aligusia kuwa ziko chanjo nyingine zinazotarajiwa na suala la msingi ni kupatikana kwake, akisisitiza haja ya kuwa na viwango vya awali na vya uhakika kudhibiti virusi vya corona na chanjo husika inatarajiwa kuruhusiwa katika nchi mojawapo kubwa na kuanza kutumika.

Anasema, itaweza kuletwa Afrika na shirika la habari la Reuters, ilijadili hotuba ya Dk. Tedros katika mkutano wa kimtandao wa mawaziri wa nchi wanachama wa WHO, wakisema kuwapo habari njema za kupatikana chanjo iliyothibitishwa kabla ya mwisho wa mwaka, mazingira ya joto Afrika, lazima yatiliwe maanani.

Pia, kuna la umbali wa kusafirisha chanjo hiyo ni mkubwa na unatakiwa ufanyike katika 'nyuzi joto kufuru' za uhifadhi, hali ambayo siyo ya kawaida katika kampeni za chanjo zinazofanywa na mashirika ya kimataifa.

Katika hali ya kawaida ya kuhifadhi na kusafirisha chanjo kwa wingi, kinachotakiwa ni uhifadhi baridi wa kawaida katika majokofu, hivyo tatizo linakuwa kukosekana umeme maeneo ya vijijini.

Shirika la kimataifa la kufuatilia masuala ya chanjo kote duniani, Gavi (Global Vaccine Alliance) lina uzoefu wa kuhakikisha kuwa majokofu yanakuwa sehemu ya maandalizi na katika maeneo mengine kunakuwapo na ulazima wa kuweka mitambo ya umeme wa jua kabla ya kufikisha vifaa na mandhari ya hifadhi ya chanjo za kawaida.

Ni wazi, maandalizi kama hayo hayawezi kutumika kwa chanjo ya Pfizer, hivyo endapo chanjo hizo zisizohitaji baridi kali kupita uwezo barani Afrika zitakubaliwa na WHO na mamlaka nyinginezo, inatazamiwa kuwa zitaweza kusambazwa huku baadaye.





# World Vision sasa yajitosa vifo vya wajawazito na watoto Bahi

**Na Paul Mabeja,** BAHI

SHIRIKA la World Vision Tanzania Kanda ya Kati limetoa msaada wa vifaa tiba kwa Hospitali ya Wilaya ya Bahi wenye thamani ya Sh. milioni 13 utakaosaidia kupunguza vifo vya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

Akipokea msaada huo Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alisema msaada huo utasaidia kupunguza vifo vya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

Alisema awali Hospitali ya Wilaya ya Bahi ilikuwa inakabiliwa na ukosefu wa vifaa tiba ambavyo vilikuwa vinakwamisha utoaji wa baadhi ya huduma za afya.

"Vifaa hivi tulivyopatiwa leo vitasaidia sana katika mapambano ya kukomesha vifo vya wajawazito pamoja na watoto chini ya miaka mitano, lengo ni kuhakikisha kuwa tunamaliza kabisa vifo katika wilaya yetu," alisema Mkunda.

Alisema, vifaa hivyo vitasaidia kuwapo kwa huduma za upasuaji ambazo zitasaidi kupunguza vifo hivyo kutokana na awali wagonjwa wengi walikuwa wakipatiwa rufani ya kwenda Hospitali ya Mkoa.

"Kupatikana kwa vifaa hivi kutasaidia kuwapo sasa kwa huduma za upasuaji katika hospitali hii ya wilaya kama kuna mtu atapata shida katika kituo cha afya ataletwa hapa umbali mfupi tofauti na ilivyo kuwa awali," alisema.

Aidha, alilipongeza Shirika la World Vision Tanzania kwa msaada wa vifaa tiba ambavyo vitasaida kuanza kutolewa kwa huduma za upasuaji.

Meneja Mradi wa kupunguza vifo vya kinamama na watoto chini ya miaka mitano, Gambo Sosthen, alisema vifaa walivyotoa ni vitanda kumi, magodoro kumi, taa kwa ajili ya kufanyia upasuaji na vifaa vya kusambazia dawa wodini.

"Mradi huu wa kupunguza vifo vya kinamama na watoto chini ya miaka mitano unatekelezwa katika wilaya za Bahi na Chemba kwa kushirikiana na halmashauri kupitia idara ya afya," alisema.

Pia, alisema mradi huo lengo lake ni kusaidi sekta ya afya pamoja na kuunga mkono juhudi za serikali kwa kuwezesha huduma mbalimbali za afya.

Pamoja na msaada huo, pia shirika hilo limetoa msaada wa vifaa mbalimbali vya ujenzi kwa ajili ya njia za watembea kwa miguu kwenye Kituo cha Afya Mundemu wilayani Bahi.



Wakazi wa Kijiji cha Membe, wilayani Chamwino, mkoani Dodoma, Aloyce Masaka (kulia) na Samwel Malima, wakisaidia kuvusha pikipiki yao kwenye korongo la maji linalotenganisha kijiji hicho na jirani cha Chitabuli, wilayani humo juzi. Eneo hilo, limekuwa kero kwa wakazi wa vijiji hivyo, hasa nyakati za mvua kutokana na kukosekana daraja. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Utafiti wafichua sababu wengi kuingia uzeeni bila maandalizi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

UTAFITI umebaini kuwa Watanzania wengi wanaingia katika maisha ya uzee bila kujiandaa kutokana na kukosa elimu ya mipango ya kustaafu.

Mtafiti Dk. Mkumbo Mitula, aliyasema hayo jana alipokuwa akikabidhi utafiti wake kwa serikali alioufanya kuhusu umuhimu wa elimu ya mipango ya kustaafu na uzee bora kwa waajiriwa na wanafunzi wa elimu ya msingi.

Alisema katika utafiti huo amebaini watu wengi wanayafikia maisha yao ya baadaye wakiwa na uelewa finyu au kukosa elimu ya uzee, na kuzeeka au hata miongozo ya kiulinzi kuhusu kuzeeka.

"Utafiti unaonyesha kuwa watu wenye mitazamo chanya kuhusu uzee wanaishi muda mrefu zaidi na wanakuwa na maisha ya afya zaidi ya wale wenye mitazamo hasi," alisema.

Alisema utafiti huo unapendekeza elimu hiyo ya mipango ya kustaafu na uzee bora inafaa ianzie kwa vijana wadogo.

"Iwapo tutawafundisha watoto kwamba kukua hadi kuwa mzee ni jambo la asili katika maisha na kuwafunda kuyapokea matokeo yenye thamani ya mchango wa wazee katika jamii, nchi na dunia tutapunguza kudhalilishwa kwa wazee," alisema.

Alibainisha kuwa elimu hiyo itasaidia kuzijenga akili za Watanzania kuwa uzee sio jambo la kupitwa na wakati au jambo lisilofaa kama dhana inavyoendelea kukua miongoni mwa vijana.

"Elimu ya uzee inaweza kuwaandaa watu kwa maisha yao yajayo na kuzuia mapambano dhidi ya uzee na wazee, lakini somo hili halionekani katika nchi yetu," alisema.

Akizungumzia matokeo ya utafiti huo, alisema watumishi wa umma asilimia 95 wanasema elimu ya mipango ya kustaafu inahitajika kwao, huku asilimia 98.3 ya wanafunzi wa elimu ya msingi na ya upili kwa pamoja wanaihitaji elimu hiyo.

Mtafiti huyo alisema utafiti huo unapendekeza mambo matatu ikiwamo kuundwa kwa timu ya pamoja miongoni mwa watafiti, watengeneza mitaala na wadau ili kuanzisha elimu hiyo.

Alitaja pendekezo lingine ni serikali iingilie kati suala la kwenye maboresho ya sera ya hifadhi ya taifa, ili sera ikidhi mahitaji yaliyopo na elimu ya mipango ya kustaafu na uzee bora liwe ni somo na liingizwe kwenye mitaala.

# Wasioona wavumbua teknolojia

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

CHAMA cha Wasioona Tanzania kimevumbua teknolojia saidizi ambayo inamsaidia mtu mwenye ulemavu wa macho kusoma maandishi yaliyoandikwa kwa wino.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Emmanuel Saimon, aliyasema hayo juzi alipokuwa akionyesha vifaa mbalimbali ikiwamo simu za mkononi na kompyuta mpakato jinsi vinavyosaidia watu wasioona kupata usaidizi kwa kupitia teknolojia hiyo ya kisasa.

Alisema ubunifu wa teknolojia hiyo ni sehemu ya mradi wa haki ya kusoma kwa wasioona ambao unaotolewa kwa ufadhili wa Shirika lisilo la kiserikali la The Foundation For Civil Society (FCs).

Alibainisha kuna teknolojia saidizi ambayo inaweza kumsaidia na kumwezesha kwa mtu asiyeona kusoma maandishi ya kawaida na yaliyoandikwa kwa wino kwa kuyapiga picha kupitia simu ya mkononi na kompyuta mpakato.

Alisema teknolojia hiyo ikiwa ni ya namna ya kumkomboa mtu asiyeona asiendelee kumtegemea mtu mwingine amsomee, lakini kwa kupitia simu yake ya mkononi na kompyuta mpakato itamsaidia kusoma maandishi ya wino yaliyopo kwenye kitabu chochote kile.

Naye, Mtaalamu wa Mawasiliano wa chama hicho, Emanuel Muhewa, alisema zamani kabla ya teknolojia hii kuwapo, watu wasioona walikuwa wakipata taabu kwenye upande wa mawasiliano katika usomaji, lakini sasa imekuwa ni mkombozi kwao.

"Zamani ilikuwa ngumu sana, hata wakati ule nikiwa nasoma shule ilikuwa ni mpaka nimuite mtu anisaidie kunisomea barua, lakini sasa hivi walau maisha yanarahisishwa... ili uweze kusoma ni lazima upakue application hii ambayo inaitwa Be my eye, hii humsaidia mtumiaji kusoma vizuri.'' Kwa upande wake Faraja Jerry ambaye pia ni mlemavu wa macho, alieleza kuwa aina ya programu wanayoitumia kwa ajili ya kutambua vitu mbalimbali yakiwamo hata mahali alipo akiwa peke yake na anaweza kutumia mawasiliano hayo kupata msaada zaidi. Alisema mfumo huo wa mawasiliano kupitia simu yake ya kiganjani unaweza kusaidia kutatua mahitaji yake yanayowezekana kwa kuwasiliana na watu wengine ukiwa peke yako kwenye eneo husika.

"Hii inamsaidia mtu asiyeona kama yuko peke yake kujua kitu anachokitafuta au anachokihitaji kiko mahali gani au kina mwonekano wa aina gani," alisema Jerry.





# Wanawake waaswa mikopo isiyo malengo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAWAKE mkoani Mbeya, wameshauriwa kuacha kuchukua mikopo kwenye taasisi za kifedha au mahali popote kama hawana malengo ya kufanya biashara au kazi za uzalishaji kwa maelezo kuwa tabia hiyo haiwasaidii kurejesha mikopo hiyo na badala yake kudidimia kiuchumi.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, wakati wa kongamano la kuwawezesha wanawake kiuchumi lililoandaliwa na Benki ya CRDB, kupitia huduma zake za Malkia Akaunti.

Alisema mara nyingi wanawake wanaochukua mikopo na kushindwa kuirejesha huwa wanafilisiwa na benki husika na mikopo hiyo inageuka kuwa shubiri badala ya msaada kuwainua kiuchumi.

Alisema kila anayechukua mkopo anatakiwa awe amejiandaa kurejesha kwa wakati ili kuepuka adhabu pamoja na kuwezesha benki husika kuwakopesha watu wengine.

"Fedha zina mambo yake na hivyo zinahitaji mipango ya uhakika, usije ukakopa fedha kwa ajili ya kununua vitenge, mwingine anachukua mkopo kwa ajili ya kula mara akisikia shangazi anaumwa anapeleka bila kujua atarejeshaje, sasa nawaomba muwe na mipango," alisema Mtunguja.

Aliipongeza Benki ya CRDB kwa kuanzisha utaratibu huo wa kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kuwa kundi hilo ni muhimu kwenye maendeleo ya familia na taifa.

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, ambaye ni miongoni mwa wanufaika wa Akaunti ya Malkia aliwataka wanawake kufanya kazi kwa bidii ili wawe sehemu ya walipakodi wazuri watakaolisaidia taifa kujiendesha.

Aliwataka wanawake wanaofanya kazi serikalini na taasisi binafsi kujianzishia miradi yao binafsi ya kuwaingizia kipato cha ziada ili wakidhi mahitaji yao na ya familia zao bila kuathiri chanzo chao cha msingi cha mapato.

"Fedha huwa hazitoshi maana kadri unavyopata nyingi zaidi ndivyo na matumizi huwa yanaongezeka, kwa hiyo ni vyema kuwa na vyanzo vingine, mimi mwenyewe nilikuwa Mkuu wa wilaya, lakini nilikuwa nasuka nywele na nina 'salon' yangu mpaka sasa inaendelea," alisema Mahundi.

Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Denis Moleka, alisema mbali na uwezeshaji huo benki hiyo pia imekuwa ikiwasaidia wanawake kushiriki mafunzo na maonyesho mbalimbali ya biashara ya ndani na nje ya nchi.

Alisema mara nyingi wamekuwa wakiwapeleka kwenye mataifa kama China na Japan, lakini mwaka huu utaratibu huo umesitishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona ambavyo vimesababisha mkwamo wa mwingiliano wa baadhi ya mataifa.

Vilevile, alisema baadhi ya wanawake wajasiriamali wamewezeshwa kuhudhuria maonyesho ya ndani kama ya biashara Dar es Salaam, Sabasaba na Nanenane.

Meneja Uhusiano Mwandamizi wa CRDB, kitengo cha uwezeshaji wanawake kutoka makao makuu, Rachael Senni, alisema CRDB Malkia ni mfumo maalumu wa kuwasaidia wanawake kiuchumi kwa kuwawezesha kuinua biashara zao.

Alisema mfumo huo una nguzo mbalimbali, lakini kubwa ni kutoa elimu ya biashara, elimu ya utunzaji wa fedha pamoja na mikopo mbalimbali kwa ajili ya wanawake hao.



Meneja Uhusiano Mwandamizi Kitengo cha Uwezeshaji Wanawake kutoka CRDB makao makuu, Rachael Senni (kulia), akimkabidhi cheti cha kutambua mchango wake Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi (katikati), wakati wa kongamano la uwezeshaji wanawake kiuchumi, jijini Mbeya juzi. Kushoto ni Meneja wa CRDB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Denis Moleka. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Madarasa 100 yanahitajika Mbeya

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

JUMLA ya vyumba vya madarasa 100 vinahitajika mkoani Mbeya, ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaotarajiwa kuanza masomo mwanzoni mwa Januari, mwakani.

Hadi sasa kuna upungufu wa vyumba vya madarasa pamoja na samani ili kuwawezesha wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaanza masomo kwa muda uliopangwa.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja kupitia kikao cha Baraza la Madiwani, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya aliagiza wakurugenzi, wakuu wa wilaya, madiwani na watumishi wa serikali kuhakikisha wanatatua tatizo la ukosefu wa vyumba vya madarasa.

"Niliomba likizo, lakini imesitishwa hii ni kutokana na tatizo lililopo la upungufu wa vyumba vya madarasa kulisimamia, hivyo kama kuna kiongozi yeyote alipanga kuomba ruhusa, asubiri mpaka tutakapolikamilisha suala hili," alisema Mtunguja.

Alisema kukamilika kwa vyumba hivyo pamoja na kununuliwa kwa viti na meza, kutasaidia wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri yenye utulivu.

Aliwahimiza viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kukamilisha haraka ujenzi wa vyumba 28 vya madarasa ambavyo vinahitajika kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2021.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Steven Katemba, aliahidi kukamilisha ujenzi huo na kuwaomba madiwani kushirikiana ili kutimiza lengo hilo.

Alisema tayari jitihada mbalimbali za kukamilisha ujenzi wa vyumba hivyo 28 zimeanza na matamanio yao ni kuona mapema Januari ujenzi wa vyumba hivyo umekamilika au kufikia hatua nzuri ya matumaini.

Mwenyekiti wa wilaya hiyo, Mwalingo Kisemba, alisema miundombinu mizuri ina mchango mkubwa katika kuongoza ufaulu kwa wanafunzi.

Alisema katika kipindi hiki madiwani watajikita uboreshaji wa miundombinu ya shule kwa kuwahamasisha wananchi kuchangia, lakini kwa serikali kuongeza bajeti.

Alisema hiyo itasaidia kuongeza ufaulu kwa watoto kwa kusoma kwenye mazingira ya utulivu na kufuatilia vyema vipindi vya masomo darasani.

## Mbaroni tuhuma wizi dizeli lita 140

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKAZI wa Kijiji cha Isnura, wilayani Mbarali, Enock Gongo (37), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuvunja nyumba na kuiba lita 140 za mafuta ya dizeli.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, aliwaambia waandishi wa habari ofisini kwake jana, mtu huyo alivunja nyumba inayomilikiwa na Tresphod Sambi, ambaye ni daktari na mkazi wa Kijiji cha Ihanga, wilayani humo.

Alisema mmiliki wa mafuta hayo alikuwa anayatumia kwenye matrekta ya kulima mashamba.

Alisema Sambi alijenga nyumba maalumu kwenye mashamba hayo kwa ajili ya kuhifadhi mafuta pamoja na vitu vingine na Gongo aliivunja nyumba hiyo na kubeba mafuta hayo na kutokomea nayo.

Kamanda Matei alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa na Polisi Desemba 7, mwaka huu akiwa ameficha mafuta hayo nyumbani kwake kwenye madumu saba ya lita 20 kila moja.

"Huyu mtu alikamatwa kufuatia msako mkali uliofanywa na polisi katika maeneo mbalimbali na alipokamatwa na kuhojiwa alikiri kuiba mafuta hayo, sasa hivi tunaendelea kumshikilia Gongo wakati uchunguzi ukiwa unaendelea," alisema Kamanda Matei.

Alisema baada ya upelelezi kukamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria huku akiwataka wananchi kuwa makini kipindi hiki cha kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka.

Aliwaonya wanaokusudia kutenda uhalifu ndani ya mkoa huo watashughulikiwa.







Kaimu Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto ambaye ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, akizungumza na wahudumu wa afya ambao ni waajiriwa wapya katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, mjini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri ahimiza viwango bora walimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amesema kuna umuhimu wa kuwaongezea walimu taaluma ili kuwasaidia wanafunzi kupata elimu bora itakayoongeza ufaulu.

Akizungumza juzi wakati alipofungua mkutano wa kujadili ripoti ya mfumo wa viwango vya elimu ya ualimu kwa wadau wa elimu katika ukumbi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, mjini Unguja, alisema lengo la ripoti hiyo ni kujua jinsi gani walimu watawafundisha watoto vizuri na kuendelea kuleta mafanikio katika sekta ya elimu.

Pia aliwataka walimu, wazazi na walezi kuwasimamia vizuri watoto ili kuhakikisha wanapata elimu bora. Naye Mkaguzi Mkuu wa Elimu wa Wizara hiyo, Dk. Rashid Abdul-aziz Mukki, alisema kuwapo kwa ripoti ya viwango vya elimu kutasaidia kukidhi haja na kusaidia walimu kuimarika zaidi katika ufundishaji na ufunzaji.

Alisema sababu za kuwapo kwa viwango hivyo zimeshaonyeshwa kupitia sera ya elimu ikiwamo kasoro na upungufu ya walimu katika ufundishaji, hivyo wizara imeshachukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha walimu wanafundisha kwa ustadi na ubunifu wa hali ya juu. Dk. Mukki alisema katika uwasilishaji wa ripoti hiyo, unalenga katika kuwatayarisha walimu wakati wakiwa vyuoni, pia viwango hivyo vinakusudiwa iwe ni mwongozo kwa wale walimu wapya wanapoingia kazini kwa kuwapatia mafunzo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Elimu Jumuishi, Mpaji Ali Maalim, alisema walimu wanapaswa kujengewa uwezo ili kuwafundisha watoto wa aina zote hata wale wenye mahitaji maalum.

Mwasilishaji wa ripoti hiyo, Profesa Bosire Monari Mwebi, aliwataka walimu wawe na njia tofauti za kufundishia watoto na kutofanya ubaguzi kwa wanafunzi pamoja na kuwaandaa vyema ili kufanya vizuri katika masomo yao.

# Walioihujumu CCM kwenye uchaguzi sasa kuwajibishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Magharibi, Mohamed Rajab Soud, ameziagiza kamati za maadili kutekeleza kazi zao kwa kuwawajibisha waliohusika kukihujumu chama hicho katika uchaguzi mkuu uliopita wa mwaka huu.

Mohamed amesema kamati za maadili zipo ngazi ya matawi, wadi, jimbo na wilaya, lakini hazijachukua hatua yoyote jambo ambalo linasababisha ugumu katika utendaji. Akizungumza juzi katika kikao cha kuwashukuru wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya za Mfenesini na Dimani, aliagiza waliotuhumiwa kuwaita katika vikao, kuwasikiliza na kutoa uamuzi unaofaa ili kupunguza malalamiko.

Pia alisema kuna baadhi ya wanachama na viongozi wameshiriki kukihujumu chama, hivyo iwapo hawatachukuliwa hatua, kutasababisha mgogoro katika chama.

Naye Katibu wa CCM Mkoa huo, Mgeni Mussa Haji, alisema uongozi wa mkoa hauwezi kumchukulia hatua mtu yoyote bila kupata vielelezi kutoka ngazi za matawi, wadi, jimbo na wilaya, hivyo kuwataka kukaa vikao na kuwatolea ripoti katika ngazi za juu ili wachukuliwa hatua za kinidhamu.

Kwa upande wao, viongozi hao waliahidi kuchukua hatua stahiki kwa yeyote atakayebainika kuwa na makosa na kuwaomba viongozi kuwachukulia hatua viongozi wanaotumia vibaya madaraka yao.

# Zanzibar, SMT sasa kufungua akaunti pamoja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamal Kasim Ali, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakaa pamoja na Serikali ya Muungano kuhakikisha inafungua akaunti ya pamoja ya kuhifadhia fedha itakayochangwa na serikali zote mbili.

Hayo aliyasema juzi Kinazini katika ziara ya kukagua taasisi zilizo chini ya Serikali ya Muungano zilizoko Zanzibar.

Jamali alitembelea ofisi za Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) zilizoko Kilimani na ofisi za Tume ya Fedha ya Pamoja zilizoko Kinazini mjini Unguja.

Alisema atahakikisha anaishauri Serikali ya Jamhuri kufanya haraka kuteua Kamishna na Katibu wa Tume ya Fedha ya Pamoja ili kurahisisha kazi za tume hiyo.

Aidha, waziri huyo aliahidi kuwapatia kiwanja cha kujenga ofisi za Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kusema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itawapa ushirikiano ili kuhakikisha huduma wanazozitoa zinakuwa na kutambulika kwa wananchi wa Zanzibar.

Pia alizishauri mamlaka hizo kutoa huduma kwa misingi ya Kiislamu ili kupata wateja wengi Zanzibar, ambapo wananchi wengi wanaoishi Zanzibar wanaishi kupitia misingi ya dini hiyo.

Aidha, alizitaka mamlaka hizo kuboresha huduma wanazozitoa na wakati mwengine kuna wadau wao hutoa risiti feki jambo ambalo huwapa usumbufu watumiaji wa huduma hiyo ya bima.

Naye Kamishna wa TIRA, Dk. Mussa Juma, alisema licha ya mafanikio yaliyopo kwenye mamlaka hiyo bado wanakabiliwa na changamoto ya watu wanaokamatwa kwa makosa ya kutokukata bima kwa watumiaji wa vyombo vya moto na ucheleweshaji wa kesi zinapofikishwa mahakamani na nyingine kuishia njiani.

Alisema wananchi wa Zanzibar wengi hawana utaratibu wa ukataji wa bima ya moto kwa nyumba wanazozimiliki au bima ya afya kutokana na ufahamu mdogo wa elimu ya bima, hivyo aliwaomba wadau wa bima na waandishi kuwapa elimu ya umuhimu wa kukata bima.

Pia alisema kwa sasa mamlaka hiyo inatarajia kutumia mfumo wa kisasa kwa mteja kupata ujumbe kupitia simu za mikononi baada ya kupata huduma unaotoka kwenye mamlaka hizo ili kuondosha usumbufu wa kupewa risiti feki kwa baadhi ya watoa huduma ambapo huduma hizo zinatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwaka ujao.

**HABARI KITAIFA**

# Mradi wa majisafi kunufaisha wajawazito

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

MRADI wa ujenzi wa tangi la maji lenye ujazo wa lita 75,000, uliogharimu zaidi ya Sh. milioni 164, na kufadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na kutekelezwa na Jukwaa la Maendeleo ya Jamii (PDF), utasaidia wajawazito 85 kwa siku na watoto wanaopata huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Halmashauri ya Mji wa Njombe, Kibena, kunufaika na huduma ya majisafi na salama.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Catalina Revocat, alisema upatikanaji wa majisafi katika hospitali hiyo, awali ulikuwa duni na kutishia afya ya wajawazito na watoto hospitalini hapo.

Alisema suala la usafi na afya katika hospitali linategemea uwapo wa majisafi na salama na utunzaji wa majitaka ambayo kama hayajashughulikiwa vizuri afya za wagonjwa zinakuwa hatarini.

Alilipongeza Shirika la UNICEF na PDF kwa ujenzi wa tangi hilo na kuisaidia serikali kuhakikisha huduma za hospitali kwa wajawazito na watoto zinakuwa nzuri.

"Hospitali hii ilijengwa muda mrefu tangu mwaka 1952 wakati huo ilikuwa ikihudumia wagonjwa wachache, lakini mji umekuwa na watu wameongezeka hivyo ilikuwa imezidiwa," alisema Catalina.

"Serikali imejitahidi kujenga miundombinu mingi, lakini suala la maji na majitaka mmekuja kutusaidia kuongeza nguvu katika juhudi zinazofanyika na serikali," alisema.

Awali, akisoma taarifa ya mradi huo, mhandisi kutoka Shirika la PDF, Elias Muchunguzi, alisema mradi huo ulianza mwaka jana mwezi Januari na kukamilika mwaka huu ambao umelenga kunufaisha watu 532.

Muchunguzi alisema kwa upande wa wodi za wazazi ambayo ndiyo kipaumbele cha mradi huo utawanufaisha wajawazito 85 kwa siku katika wodi tatu za wazazi hospitalini hapo.

Wanufaika wengine wa mradi huo ni wagonjwa wa wodi za kawaida na wafanyakazi wa hospitali hiyo ambao ni zaidi ya 187.

"Zaidi ya Sh. milioni 160 zimetolewa na mfadhili, lakini kwa halmashauri imechangia Shilingi milioni nne na kufanya mradi huo kukamilika kwa zaidi ya Sh. milioni 164," alisema Muchunguzi.

Mwakilishi wa UNICEF, Pamela Shao, alishukuru kwa maendeleo ya hospitali hiyo na adha ya maji kutatuliwa.

# RC atembelea kiwanda kujifunza uendeshaji machinjio Vingunguti

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge, ametembelea kiwanda cha kisasa cha uchinjaji na usindikaji wa nyama cha TanChoice kilichoko Soga, Kibaha mkoani Pwani kwa lengo la kujifunza na kupata uzoefu utakaowezesha kuboresha machinjio ya kisasa ya Vingunguti.

Katika ziara hiyo aliyoifanya jana, Kunenge aliambatana na watendaji kutoka Manispaa ya Ilala, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na watendaji wa ofisi yake kujionea hatua zote za uchinjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo kuanzia hatua ya kwanza hadi ya mwisho.

Akizungumza baada ya kufika kiwandani hapo, Kunenge alionyesha kuridhishwa na namna kiwanda hicho kinavyozalisha nyama kwa viwango vya kimataifa jambo linalosababisha asilimia 80 ya nyama inayozalishwa kiwandani hapo kuuzwa nje ya nchi.

Kunenge aliupongeza uongozi wa kiwanda hicho kwa kutafsiri kwa vitendo ndoto ya Rais John Magufuli ya Tanzania ya viwanda, jambo lililowezesha kutoa ajira na kuchangia ukuaji wa uchumi.

Alisema kiwanda hicho pia kitasaidia wafugaji kutoka mikoa mbalimbali nchini kupata soko la uhakika la kuuza mifugo yao kwa bei yenye tija.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda hicho, Rashid Abdilah, alisema kwa sasa kiasi kikubwa cha nyama wanayozalisha wanaiuza Umoja wa Falme za Kiarabu, Oman, Qatar na Kuwait na kueleza kuwa mahitaji ya nyama nje ya nchi bado ni makubwa.




Meneja Rasilimali Watu wa Kampuni ya Tanzania Distilleries Limited (TDL), Mariam Kambinga, akimkabidhi mmoja wa wafanyakazi wa kituo cha kulea watoto yatima cha Maria Theresa kilichopo Mburahati jijini Dar es Salaam, Mary Mathias (watatu kulia) msaada wa chakula uliotolewa na wafanyakazi wa kampuni hiyo kituoni hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ongezeko wanawake wasio na wenza latisha

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

IDADI ya wanawake wanaoishi bila wenza kutokana na kufariki dunia au kuachika imezidi kuongezeka jambo ambalo ni hatari kwa ustawi wa familia na jamii kwa ujumla.

Kutokana na hali hiyo, Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Delvin Maleko, amesema kuna haja ya kutoa elimu kwa wanaume na wanawake kuhusu wajibu wa kulea familia ili kuokoa udumavu wa akili na kimwili kwa watoto.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa akifungua semina ya siku moja kwa wanawake wasio na wenza iliyoandaliwa na asasi ya Tanzania Marriage and Child Care (TaMCare), inayojishughulisha na masuala ya ndoa na malezi ya watoto.

Maleko alisema idadi kubwa ya wanawake wa wilaya hiyo, wanaoachiwa majukumu na wanaume hali zao za kimaisha ni duni, hivyo kuwalea watoto wao katika mazingira magumu ambayo ni hatari baadaye.

"Hali ya watoto kulelewa na mzazi mmoja imekuwa kisababishi cha kudumaa kimwili na kifikra. Tukiendelea hivi tutakuwa na taifa lenye watoto waliodumaa. Kujikomboa katika hili ni kufanya semina kwa wanaume na wanawake," alisema.

Maleko alisema katika kata za Dunda na Magomeni wilayani Bagamoyo, wanawake wanaoishi bila waume ni 505 na wamepewa mzigo mkubwa wa kulea familia huku watoto wanaowalea ni zaidi ya 1,500.

Alisema chanzo cha uwapo wa idadi kubwa ya wanawake hao ni kutokana na waume zao kufariki dunia pamoja na mila na desturi ambazo baada ya kufanyika watoto wa kike, wamekuwa na mabadiliko yanayosababisha kupata mimba mapema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TaMCare, Mchungaji, Dk. Enock Mlyuka, alisema shirika hilo limeamua kuelekeza nguvu kwa wanawake wanaoishi bila wenza wao kutokana na umuhimu wa kundi hilo katika jamii ili kuepuka athari ambazo zinaweza kutokea baadaye kwa kuwa na watu wasiojitambua na ongezeko la mmomonyoko wa maadili.

Mlyuka alisema tayari TaMCare imewafikia wanawake wasio na wenza ambao wanaishi katika mazingira magumu 505 katika Wilaya ya Bagamoyo na watoto 1,543 wanaotunzwa na wanawake hao.

"Wengi wa wanawake hao wameachika na kutelekezwa. Wanaachiwa kulea familia peke yao na wengi wao wamejikuta wakipoteza umakini na kujiingiza katika mahusiano (uhusiano) yasiyo (usio) salama. Hali hii imesababisha msongo wa mawazo, hivyo kuathiri makuzi na afya za watoto," alisema.

Alisema shirika hilo limekusudia kuwasaidia wanawake hao kwa kuwaongezea ufahamu na maarifa ili kubadili tabia, mienendo na mitazamo isiyofaa kuhusu maisha, kutambua haki zao na kuwawezesha kiuchumi ili kuboresha hali yao kimaisha na watoto wao.

# Mdau aunga mkono ajira walimu wa ziada

**Na Mwandishi Wetu,**

SHINYANGA

KATIKA kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha sekta ya elimu na kuboresha mazingira ya kujifunzia, kampuni ya uhandisi wa umeme na mitambo ya viwandani pamoja na migodini ya Magare ya jijini Mwanza, imeajiri walimu wa ziada sita.

Aidha, imekamilisha mfumo wa maji kwenye Shule ya Sekondari Isagehe iliyopo wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Hatua hiyo imeenda sambamba na makabidhiano ya msaada wa vifaa vya shule ikiwamo kompyuta, mashine za photocopy na kuprint zilizotolewa na kampuni ya hiyo kwa ajili ya kusaidia walimu wa shule hiyo katika kufanikisha shughuli zao za kiofisi ikiwamo maandalizi ya mitihani.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano hayo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Magare, Mabula Magangila, alisema msaada huo unafuatia ombi la walimu na wanafunzi wa shule hiyo walilotoa kwake siku chache zilizopita alipoalikwa kwenye mahafali ya kidato cha nne ya shule hiyo.

"Binafasi niliguswa zaidi kushirikiana na shule hii kutokana na sababu kadhaa ikiwamo uhusiano nilionao na shule hii ambapo ndipo nilipopata elimu yangu ya sekondari, tena kwa msaada mkubwa wa walimu wa ziada kama hawa," alisema na kuongeza:

"Pia kampuni yetu inafanya shughuli zake katika maeneo haya, hivyo ni vema tutoe sehemu ya faida yetu kwa jamii iliyotuzunguka."

Akizungumzia walimu sita waliojariwa na kampuni hiyo kwa ajili ya kufundisha katika shule hiyo, Magangila alisema kati yao watatu ni wa masomo ya sayansi na watatu ni wa masomo ya biashara, huku akiongeza kuwa wameshaingizwa kwenye orodha ya malipo kupitia kampuni ya Magare kuanzia Januari mwakani.

"Walimu hawa wataendelea kulipwa na Kampuni ya Magare hadi pale watakapoingizwa kwenye ajira rasmi ya serikali. Lengo ni kuboresha ufaulu mapema iwezekanavyo," alisema.

Aliuomba uongozi wa shule hiyo kuvitumia ipasavyo vifaa vya ofisi viliyotolea na kampuni hiyo ili viweze kuwasaidia katika uandaaji wa mitihani na maandalizi mengine ya masomo.

Aliongeza kuwa licha ya serikali kuelekeza nguvu nyingi katika kuboresha elimu nchini, ipo haja ya sekta binafsi kuunga mkono jitihada hizo kwa kusaidia maeneo mbalimbali ikiwemo ujenzi wa madarasa na ununuzi wa vifaa vya kujifunzia ikiwemo kompyuta na vinakilishi.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya uhandisi wa umeme na mitambo ya viwandani na migodini ya Magare ya jijini Mwanza, Mabula Magangila (katikati), akikabidhi msaada wa vifaa vya shule zikiwamo kompyuta, mashine za kuchapisha na kinukuzi, zilizotolewa na kampuni hiyo, kwa ajili ya kusaidia walimu na wanafunzi wa Shule ya ya Sekondari Isagehe, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga jana. Kushoto ni Mkuu wa shule hiyo, Adolf Kabyemela. **MPIGAPICHA WETU**.

# Soko jipya Njombe rasmi Januari Mosi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Ruth Msafiri, amesema soko jipya lililojengwa wilayani hapo kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni tisa na serikali litaanza rasmi Januari mosi, 2021.

Akizungumzia mkakati wa serikali kuhusu matumizi ya soko hilo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi, Ruth alisema tayari tangazo la Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe kuwataka wananchi kuomba maeneo ya kufanyia biashara ndani ya soko hilo, limetolewa na kuwataka wafanyabiashara kujitokeza kuomba nafasi.

Alisema kwa mujibu wa tangazo hilo, ada zitakazotolewa na mwombaji ni Sh. 30,000 kwa wafanyabiashara watakao omba maduka ya kufanya biashara na Sh. 1,000 moja ambazo zitalipwa kupitia namba maalum iliyoteuliwa.

"Soko hili tofauti na nyakati nyingine zote lina miundombinu yote na kwa hiyo tunapendekeza kwa vyombo vyetu vya ngazi ya juu watukubalie tunataka soko letu lifanye kazi saa 24, iwe ni kituo cha biashara cha Njombe mjini si soko tu, bali kituo cha biashara," alisema Ruth.

Pia, alitoa angalizo kwa wanaoomba kupatiwa meza na maduka kutofanya vitendo vyovyote vya kushawishi au kutoa rushwa.

Kwa mujibu wa mkandarasi aliyejenga soko hilo, lina jumla ya vyumba 162 pamoja na meza za wajasiriamali wadogo 424.

Kipaumbele kitawalenga wafanyabiashara zaidi ya 500 ambao walikuwa wakifanyabiashara kwenye eneo la soko hilo kabla ya kuvunjwa la kwanza ili kupisha ujenzi wa soko jipya.

Naye mmoja wa wafanyabiashara mjini Njombe Christina Nyagawa, alisema wanaipongeza serikali kwa kukamilisha ujenzi wa soko hilo jipya ambalo litawafanya kuwa uhuru kufanya biashara katika maeneo yanayoweza kufikiwa na wateja wao kirahisi tofauti na sasa.

# RAS awaonya wasaidizi sheria

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

SERIKALI mkoani Morogoro imewataka watoa huduma za kisheria mkoani humo kujiepusha na vitendo vya kupindisha sheria, ili kujipatia fedha kinyume na utaratibu hali ambayo inachangia kuwapo kwa migogoro katika jamii.

Rai hiyo ilitolewa jana na Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Emmanuel Kalobero, katika kongamano la kituo cha wasaidizi wa huduma za kisheria la Morogoro Paraligal Center, kutathmini utekelezaji wa mradi wa miaka minne wa kuisaidia jamii masuala ya kisheria.

Alisema kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya jamii kuhusu vitendo vinavyofanywa na baadhi ya wanasheria kupindisha sheria kwa makusudi jambo linalochangia kwa ongezeko la migogoro ya ardhi na ukatili wa kijinsia.

"Msitumie uelewa wenu wa kisheria kuwa vishoka wa kisheria kwasababu heshima yenu sio kupindisha haki ya mtu bali kusaidia watu kuondokana na hizi changamoto za unyanyasaji wa kijinsia, mimba za ututoni, lakini hata migogoro ya ardhi siyo kwenda kinyume kisa mnajipatia fedha," alisema Kaloboro.

Kwa upande wake Mratibu wa msaada wa kisheria Morogoro, Augustino Ernest, alisema mradi huo umelenga kuisaidia jamii kutambua namna ya kudai haki kwa kutumia sheria.

Alisema katika utekelezaji wa mradi huo, tatizo ni asilimia kubwa ya wananchi hasa maeneo ya vijijini kutokuwa na elimu ya kisheria jambo lililosababisha wengi wao kukosa haki zao za msingi.

"Mkoa wa Morogoro bado kuna changamoto ya ukatili wa kijinsia, watoto wanapata mimba za ututoni wengine wanaachishwa shule wakaolewe, sasa pamoja na kuwafikia walengwa, lakini wengi hawana elimu ya sheria kwa hiyo baadhi wanashindwa kutoa ushirikiano wakihofia kuvunja mahusiano katika familia zao," alisema Ernest.

Baadhi ya watoa huduma za kisheria kwenye wilaya mbalimbali walio chini ya kituo cha huduma za kisheria cha Morogoro Paraligal Center, walisema pamoja na tatizo la elimu, jitihada zinaendelea ili kuhakikisha wananchi wanapata haki zao.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria, Wilaya Malinyi, Rashidi Ally, alisema awali walikuwa wanapata wakati mgumu kuwaelimisha wananchi kuwa mstari wa mbele kudai haki zao na sasa imeanza kuelimika.



# Ronaldo: Juve haina cha kuhofia kwa sasa

**BARCELONA,** Hispania

CRISTIANO Ronaldo amesema Juventus hawana cha "kuhofia" baada ya kutawala mchezo wakati wakiifunga Barcelona mabao 3-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi, Jumanne.

Ronaldo alifunga kwa penalti vipindi vyote viwili wakati mpinzani wake, Lionel Messi akiwa kwenye wakati mgumu ushindi ambao ulitosha kuwafanya Juve kuwapiku Barca kileleni mwa msimamo wa Kundi G.

Kabla ya mchezo huo, timu zote mbili zilikuwa zimeshafuzu hatua ya mtoano wa timu 16-bora kwenye michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Baada ya mchezo huo, Ronaldo mwenye umri wa miaka 35, aliwaambia waandishi wa habari kwamba ushindi ulikuwa jambo muhimu zaidi kwa Real Madrid.

"Mara zote najisikia fahari kurudi Hispania na Catalunya. Mara zote ni ngumu sana kucheza Camp Nou dhidi ya moja ya timu bora zaidi niliyowahi kuikabili," alisema Ronaldo.

"Leo (juzi) tulikuwa timu ya mabingwa! Timu ya kweli imara na iliyoungana kama familia!

"Kucheza kama hivi, hatuna cha kuhofia hadi mwisho wa msimu huu, twende zetu."




# Inter yawania beki wa Barca

**MILAN,** Italia

KLABU ya Inter Milan inawania kumsajili mlinzi wa Barcelona, Junior Firpo wakati wa dirisha dogo la Januari, kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Hispania.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, hana nafasi pale Nou Camp na ripoti zinadai kwamba amewashiwa taa ya kijani kuondoka kipindi cha dirisha dogo la usajili la Januari.

Na kwa mujibu wa Diario Sport, miamba hao wa Serie A wapo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili mlinzi huyo wa kushoto, Firpo, huku kocha Antonio Conte akiripotiwa kwamba anavutiwa zaidi na mchezaji huyo.

Hata hivyo, Conte anamtaka mchezaji huyo kuanza kwa mkopo kabla ya kumpa mkataba wa kudumu klabuni hapo.

Ripoti hiyo imeongeza kuwa klabu za Atalanta na Napoli pia zinawania saini ya mchezaji huyo, lakini Inter ndio wenye nafasi kubwa zaidi.

Awali Firpo alikaribia kutua kwa miamba hao wa dimba la San Siro katika uhamisho ambao ungemhusisha straika wa Inter, Lautaro Martinez kwenda Barcelona, lakini dili hilo lilishindikana dakika za mwisho.

Mchezaji huyo wa zamani wa Real Betis amecheza mechi tano kwa Barcelona iliyopo chini ya Ronald Koeman kwa msimu huu wa 2020-21, akicheza kwa dakika 192 msimu huu.

# PSG yavunja mkataba na Rodriguez




**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain ya Ufaransa imesitisha mkataba wa mshambuliaji kutoka nchini Hispania, Jese Rodriguez Ruiz, ambao ulikua umesalia miezi sita kabla ya kufika kikomo.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alisajiliwa PSG mwaka 2016 akitokea kwa mabingwa wa soka nchini kwao Hispania, Real Madrid mwaka 2016, lakini alipelekwa kwa mkopo katika klabu nne tofauti.

Jese ametumika mara mbili kwenye kikosi cha PSG msimu huu akitokea benchi kwenye michezo ya Ligi ya Ufaransa.

Lakini, baada ya kukabiliwa na changamoto kadhaa ya nje ya uwanja katika siku za karibuni, PSG wameamua kukatisha mkataba wake.

PSG wamethibitisha taarifa hizo kupitia tovuti yao rasmi: "Paris Saint-Germain inamtakia Jese heri katika kipindi chote cha kuendelea kucheza sehemu nyingine."

Jese anaondoka Mji Mkuu wa Ufaransa, Paris, akiwa amefunga mabao mawili katika michezo 18 kwenye mashindano yote.

## HABARI MICHEZO



# Griezmann: Barca tuna kazi ya ziada

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi alipiga mashuti saba yaliyolenga goli bila kufunga wakati Barcelona ikichezea kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Juventus kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku Antoine Griezmann akibainisha hilo ni kama kuwafanya waamke.

Messi alikuwa akipambana kutaka kuirudisha Barca mchezoni kwa kujaribu kutumia uwezo wake binafsi, lakini mambo yalikuwa magumu kwao.

Nyota huyo aligusa mpira mara 125 ikiwa mara nyingi zaidi kuliko mchezaji yeyote kwenye mchezo huo uliopigwa katika dimba la Camp Nou.

Messi alipiga mashuti 11, saba yalilenga goli, lakini hakuweza kumfunga golikipa mkongwe wa Juve, Gianluigi Buffon.

Badala yake alikuwa ni mpinzani wake Cristiano Ronaldo ambaye aliwawezesha Juve kupaa kileleni mwa msimamo wa Kundi G, akifunga penalti mbili katika kila kipindi.

Hayo yaliyokuwa mabao ya kwanza kwa Ronaldo dhidi ya Barca kwenye mashindano hayo baada ya kutoka sare katika mechi tano.

Hata hivyo, Messi ndiye alikuwa mchezaji pekee wa Barca ambaye alimjaribu mara nyingi zaidi Buffon, huku Martin Braithwaite naye akijaribu mara mbili.

Griezmann baada ya mchezo huo alitoa ya moyoni na kusema kwamba, imewafanya waamke.

"Hakukuwa na morali. Kila kitu kilikuwa kibaya," alisema na kuongeza kwamba ulikuwa mchezo mbaya zaidi kwako.

"Wachezaji ndio wa kulaumiwa, sisi ndio tunaocheza na tunatakiwa kujituma. Tunatakiwa kushinda mchezo wa Jumapili dhidi ya Levante, kwa sababu mambo yamekuwa magumu kwa upande wetu."

## Sabella wa Argentina amfuata Maradona

**BUENOS AIRES,** Argentina



MCHEZAJI wa zamani wa Leeds United na Sheffield United na kocha wa zamani wa Argentina, Alejandro Sabella amefariki dunia katika umri wa miaka 66.

Sabella, ambaye aliiongoza nchi yake ya Argentina kutinga fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2014, alilazwa hospitali tangu Novemba mwaka huu.

Aliichezea Sheffield mechi 76 kati ya mwaka 1978 na 1980 kabla ya kujiunga na Leeds, ambako alicheza mechi 23.

Kifo chake kimekuja wiki mbili tu baada ya kifo cha mchezaji na kocha wa zamani wa Argentina, Diego Maradona.

Twitter ya Chama cha Soka cha Argentina, ilisomeka: "Familia ya Chama cha Soka cha Argentina inatangaza kifo cha Alejandro Sabella, na kinatoa pole kwa familia na ndugu wote."

Sabella alijiunga Sheffield United akitokea River Plate baada ya klabu hiyo kushindwa kumsajili Maradona.

Alirudi nyumbani kwao baada ya muda mfupi pale kwenye dimba la Elland Road na akajiunga Estudiantes, ambapo baadaye alikuwa kocha wake na kuiwezesha kutwaa taji la Copa Libertadores (Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini) mwaka 2009.

Kazi yake ya ukocha wa timu ya Taifa ya Argentina ambaye aliichezea mechi nane, ilianza mwaka 2011 na kumalizika baada ya fainali za Kombe la Dunia mwaka 2014 nchini Brazil, ambapo walifungwa na Ujerumani.

# Ozil Uturuki sasa muda utaongea

**ANKARA,** Uturuki

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil, huenda akaondoka kaskazini mwa Jiji la London na kutimkia nchini Uturuki kujiunga na klabu ya Fenerbahce.

Ozil ambaye amekuwa na wakati mgumu ndani ya kikosi cha Arsenal kutokana na jina lake kuenguliwa kwenye usajili wa kikosi cha Ligi Kuu na michuano ya kimataifa, anahusishwa na taarifa hizo, huku ikielezwa usajili wake utakamilishwa Januari 2021.

Taarifa kutoka kwa rafiki wa karibu na kiungo huyo aliyejiunga na Arsenal mwaka 2013



akitokea kwa mabingwa wa Hispania, Real Madrid, Murat Zorlu zinasema, kuna asilimia 90 kwa Ozil kuondoka London.

"Nina uhakika kwa asilimia 90 Ozil atakuja Uturuki kwenye dirisha la usajili la Januari. Chanzo kilichopo karibu zaidi na klabu kimenieleza kuwa Ozil anauwezekano mkubwa wa kuwa mchezaji wa Fenerbahce kwenye dirisha la usajili lijalo. Ninaweza kusema asilimia 90 atajiunga na sisi mwezi ujao," Zorlu aliimbia Sport Digitale.

Ozil amekuwa akihusishwa na timu za Uturuki kwa muda sasa, inasemekana ana wafuasi wengi wanaomshabikia nchini Uturuki. Pia, mke wa Ozil alikuwa Miss Uturuki mwaka 2014 na Ozil mwenyewe anaasili ya Uturuki.

Tangu kuondoka kwa Arsene Wenger, Ozil amekuwa na maisha magumu ndani ya klabu ya Arsenal.

Meneja aliyeajiriwa baada ya kuondoka kwa babu huyo kutoka nchini Ufaransa, Unai Emery alishindwa kumtumia kiungo huyo aliyekuwa sehemu ya kikosi cha Ujerumani kilichotwaa ubingwa wa Kombe la Dunia mwaka 2014, kwenye kikosi cha Arsenal, hali kadhalika kwa meneja wa sasa Mikel Arteta.

Katika msimu wa mwisho wa Wenger kukinoa kikosi cha Arsenal, Ozil alisaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia Arsenal na aliongezewa mshahara na kufikia pauni 350,000 kwa wiki, huu ni mshahara mkubwa zaidi ukilinganishwa na mishahara ya wachezaji wengine wote wa klabu hiyo.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOLSKAJAER SASA ATEMA NYONGO BENCHI POGBA

●●● Ni uamuzi wa kiufundi, tuliamua kwa Scott McTominay na Nemanja Matic, tunaangalia...

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amesisitiza uamuzi wa kumwanzishia benchi Paul Pogba wakati Manchester United ikichapwa na RB Leipzig kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ulifanywa "kabla ya mchezo" huo.

Pogba alianzia benchi juzi Jumanne wakati Man United ikifungwa mabao 3-2 na RB Leipzig na kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi.

Pogba aling'ara kwenye mchezo wa ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya West Ham kwenye mchezo wa Ligi Kuu Jumamosi, lakini aliachwa kwa timu hiyo wakati ikiwavaa miamba wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Leipzig, Jumanne baada ya wakala wake, Mino Raiola, kudai kwamba mchezaji huyo hana furaha pale United na anatakiwa kuondoka wakati wa dirisha lijalo.

Raiola aliliambia gazeti la Italia la Tuttosport kwamba Pogba anaweza kurudi Juventus akiwa anahitaji "kubadili hewa".

**Kauli yake ilikuja saa chache kabla ya United , ambao walikuwa wanahitaji pointi moja kwenye mchezo dhidi ya Leipzig ili ifuzu hatua ya mtoano wa timu 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo sasa itavaana na Manchester City kwenye Ligi ya England mwishoni mwa wiki ijayo.**

Pogba, ambaye amecheza mechi 13 kwenye mashindano yote msimu huu, alikuwa mmoja wa wachezaji watano ambao walifanyiwa mabadiliko na Solskjaer.

"uamuzi wetu ulikuwa wa kiufundi," alisema Solskjaer akiiambia BT Sport. "Hicho ndicho kitu pekee. Tunahitaji maamuzi kufanyika kabla ya mchezo.

"Tuliamua kwa Scott McTominay na Nemanja Matic katika kiungo kabla ya mchezo dhidi ya West Ham. Mara zote tunafikiria kuhusu ubora wa wachezaji 11."

Alipoulizwa kuhusu athari ya kauli za Raiola, Solskjaer alijibu: "Hakuna. Unajiandaa katika kila mchezo kama ndio mchezo wao wa mwisho. Tutacheza na City Jumamosi.

"Hilo halimaanishi kwamba huo mchezo ni wa kwetu kirahisi kwa sasa.

"Jambo la muhimu kwa sasa ni kwamba, timu itakuwa ikifanya vizuri na si kusikiliza nani anasema nini."

## KWA UFUPI

### MILAN KUUZWA SPURS
KLABU ya Inter Milan inajiandaa kumuuza mlinzi, Mslovakia Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 25, kwa Tottenham kwa pauni milioni 45 mwezi ujao. (Sun)

### SCHUURS AIPOTEZEA LIVERPOOL
BEKI wa kati wa Uholanzi, Perr Schuurs mwenye umri wa miaka 21, aliyehusishwa na taarifa za kuhamia Liverpool, amesisitiza kuwa hayuko tayari kuondoka Ajax. (Mirror)

### POCHETTINO AONGOZA MADRID
KOCHA wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino, anaongoza mbele ya kocha wa kikosi cha akiba cha Real Madrid, Raul kama mmoja anayepewa nafasi kubwa ya kuchukua nafasi ya Zinedine Zidane, iwapo Real wataamua kumfuta kazi Mfaransa huyo. (Marca)

### MOYES NA MKATABA MPYA
KLABU ya West Ham ipo katika mazungumzo na kocha David Moyes kuhusu kuongezwa kwa mkataba wake, ambao unamalizika msimu huu. (Sky Sports)

### ZIDANE HAJUI KUHUSU HAZARD
KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amepoteza imani na wachezaji wake kadhaa akiwamo winga wa zamani wa Chelsea, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 29, ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Ubelgiji. (Sport)

### TERRY KUMPA ULAJI COLE
KOCHA msaidizi wa Aston Villa, John Terry, atamtafuta mchezaji mwenzake wa zamani wa Chelsea, Ashley Cole kushikilia nafasi ya kazi katika utawala wake wa timu kama atateuliwa kurithi mikoba ya Phillip Cocu. (Mirror)

### MOURINHO KUAMUA KWA DELE
KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho, anasema ni jukumu lake kuamua iwapo klabu hiyo itamuuza kiungo wa kati wa England, Dele Alli mwenye umri wa miaka 24, wakati wa dirisha la usajili la Januari au la. (Telegraph)

### NEWCASTLE YAMTAKA WILLIAMS
KLABU ya Newcastle imekuwa ikimfuatilia kwa karibu mchezaji wa Manchester United, Brandon Williams huku kijana huyo mwenye umri wa miaka 20, anayecheza nafasi ya mlinzi wa kushoto katika kikosi cha vijana walio chini ya umri wa miaka 21 cha England, anaweza kupatikana kwa mkataba wa mkopo Januari. (Newcastle Chronicle)

### ARTETA AJIPANGA JANUARI
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema yeye pamoja na Mkurugenzi wa Ufundi, Edu wanafanya mpango kwa ajili ya kipindi cha dirisha la uhamisho la Januari na kile kinachoweza kuwa soko 'lisilotarajiwa'. (London Evening Standard)

### BREMEN HAIMUUZI RASHICA
KLABU ya Werder Bremen imeachana na mpango wa kumuuza kiungo wake wa kati, Milot Rashica dirisha la Januari licha ya taarifa kwamba, Aston Villa wanaweza kurejelea nia yao kwa kijana huyo mwenye umri wa miaka 24. (Birmingham Mail)

HABARI MICHEZO

# KLABU LIGI KUU BARA ZAMGOMBEA ILANFYA

**Na Saada Akida**

KATIKA kuimarisha kikosi chake kuelekea usajili wa dirisha dogo, mabosi wa Coastal Union wanajipanga kupeleka maombi kwa mabingwa watetezi, Simba ili kumpata kwa mkopo mshambuliaji wao, Charles Ilanfya.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Coastal Union, Steven Mnguto, alisema kulingana na mwenendo wa timu yao katika mzunguko wa kwanza, wameona kikosi chao kina upungufu na sasa wanasubiri rasmi mapendekezo ya benchi lao la ufundi.

Mnguto alisema katika mapendekezo ya awali ni kutafuta mshambuliaji na kuhusu Ilanfya wanafikiria kupata huduma ya nyota huyo ambaye anawindwa na timu nyingine zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania.

"Ni mchezaji mzuri na atatufaa, kwa mahitaji ya timu yetu, atatusaidia lakini bado hatujapeleka maombi yoyote Simba, ila ni mchezaji ambaye anawindwa na timu mbalimbali, kikubwa tunasubiri mapendekezo ya mwalimu wetu," alisema Mnguto.

Aliongeza bado hawajaanza kusajili ila wapo katika mchakato wa kuangalia wachezaji ambao watawaongeza katika dirisha dogo kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chao kuelekea hatua ya mwisho ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ilanfya ni miongoni mwa wachezaji wa Simba ambao wanatajwa watatolewa kwa mkopo kipindi cha dirisha dogo linalotarajiwa kufunguliwa ifikapo Desemba 15, mwaka huu.

Mshambuliaji huyo amekosa namba katika kikosi cha kwanza cha mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambacho kiko chini ya kocha Sven Vandenbroeck na Suleiman Matola.

Mbali na Coastal Union, timu nyingine zinazotajwa kuhitaji huduma ya mshambuliaji huyo aliyesajiliwa na Wekundu wa Msimbazi hao akitokea KMC FC msimu uliopita ni Ihefu FC ya jijini, Mbeya ambayo kwa sasa inaburuza mkia.

VIPIMO...



Bondia Abdallah Pazi maarufu Dulla Mbabe (kulia), akipimwa na madaktari kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), ikiwa ni sehemu kuadhimisha miaka 59 ya Uhuru. Bondia huyo anatarajia kucheza pambano la Usiku wa Mabingwa Desemba 26, mwaka huu. **MPIGAPICHA WETU**.

# Kituo cha kimataifa kujengwa Singida

**Na Jumbe Ismailly, SINGIDA**

KAMATI ya Olimpiki Afrika kwa kushirikiana na Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), wameingia makubaliano ya kujenga Kituo cha Kimataifa cha Michezo kwenye eneo la Kijiji cha Sagarumba, kilichoko Wilaya ya Singida Mjini mkoani hapa.

Makubaliano hayo yalifanyika rasmi jana kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Singida yakiwahusisha viongozi wa TOC.

Akizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo, Rais wa TOC, Ghulamu Rashid, alisema ujenzi wa kituo hicho utakapokamilika utakuwa na viwanja vya ndani, hosteli, riadha, mpira wa kikapu, netiboli, na viwanja vya michezo ya watoto.

"Kwa hivyo tunaamini kabisa kwamba katika mwendelezo wa shughuli hizi tutafanikiwa katika kuhakikisha tunajenga kituo na tutakiita Sports Complex, kituo chenye michezo mingi kwa pamoja," alisema Rashid.

Kiongozi huyo aliweka wazi awali mpango wa kujenga kituo kama hicho ulipangwa kufanyika kati ya Kibaha na Bagamoyo mkoani Pwani, lakini kwa zaidi ya miaka 14, lilikosekana eneo la kujenga mradi huo.

Alieleza Singida imekuwa na bahati ya kupata kituo hicho kama ambapo tayari Zambia wameshapata baada ya kupatikana kwa eneo mapema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alisema mbali na kituo hicho kutarajiwa kutumiwa kwa ajili ya michezo, lakini kitakuwa ni kituo cha kutoa mafunzo mbalimbali kwa vijana.

Kituo hicho kinatarajiwa kujengwa kwenye eneo la ukubwa wa hekari 29 na kitajengwa katika Kijiji cha Sagarumba, kilichoko Kata ya Merya wilayani Singida.

# Simba Queens waitisha Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amewataka wachezaji wake kuendeleza ubabe dhidi ya watani zao, Yanga Princess katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

Mgosi alitoa kauli hiyo baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya JKT Queens katika mchezo mwingine wa ligi hiyo uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Simba Mo Arena jijini.

Kocha huyo alisema amewakumbusha wachezaji wake kujipanga kusaka ushindi na kutokubali watani zao kuwafunga kwa mara ya kwanza, huku wakiwa wanaongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Sisi tupo chini kwenye msimamo, tunahitaji kupanda mlima, tumefanikiwa kupata pointi tatu dhidi ya JKT Queens, sasa tuna kazi ya kuhakikisha tunaenda kupata pointi tatu muhimu nyingine dhidi ya Yanga Princess ambao wapo juu yetu, malengo yetu ni kupanda juu ya msimamo," alisema Mgosi.

Aliongeza anawaheshimu Yanga Princess ambao msimu huu wamejiimarisha, lakini anawafahamu wachezaji wao na anajiandaa kuwafundisha soka la kisasa.

"Najua Yanga Princess wamejiimarisha, katika mpira wa wanawake kwa sasa lazima uzitaje Simba na Yanga, nina amini kwa uimara wao waliokuwa nao tunahitaji pointi tatu ila wajitahidi kupunguza idadi ya mabao saba au matano ambayo tulikuwa tukiwafunga kwa misimu iliyopita," alisema Mgosi.

# Ben Pol akiweka 'Kidani' videoni

**Na Mwandishi Wetu,**

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Behnam Paul a.k.a Ben Pol, ameachia video ya wimbo uitwao Kidani ambao amemshirikisha mkewe Anerlisa, ameeleza.

Akizungumza na gazeti hili, Ben Pol alisema wimbo huo ameutambulisha jana siku ambayo Tanzania inasherehekea uhuru wake ambao ulipatikana Desemba 9, mwaka 1961.

Ben Pol alisema amewapa mashabiki wake zawadi nzuri ya kufungia mwaka 2020 na kumtaja mtayarishaji Hanscana ndiye aliyeutengeneza wimbo huo.

Alisema video ya kibao hicho imefanyika jijini Dar es Salaam na imetambuliwa katika kipindi ambacho kuna sintofahamu ya ndoa yake baada ya kuwapo kwa tetesi kwamba imevunjika.

"Video hii inaweza kuwa ni uthibitisho kwamba ndoa yangu na Anerlisa bado iko imara, pia ninaendelea kutoa shukrani za dhati kwa mashabiki wangu kwa ushirikiano wanaonipa na nimeona niandae burudani kwao," alisema msanii huyo.

Alisema ameandaa usiku maalum utakaofanyika Desemba 31, mwaka huu kwenye Hoteli ya Ramada kwa lengo la kuuzindua wimbo huo.

Alhamisi Desemba 10, 2020
Nipashe

# Michezo


HABARI UK.22

## Solskajaer sasa atema nyongo benchi Pogba

## Magufuli amtaka waziri kumulika vipigo Taifa Stars

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amewaeleza Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa na Naibu wake, Abdallah Ulega, kuwa hatasita kuwatumbua endapo timu za taifa ikiwamo Taifa Stars zitaendelea kufanya vibaya katika michuano mbalimbali.

Akizungumza jana jijini Dodoma wakati akiwaapisha mawaziri 21 na manaibu mawaziri 22 aliowateua Desemba 5, mwaka huu, Rais Magufuli alisema endapo timu ya taifa itafungwa mabao 10, Bashungwa ataondoka na Naibu Waziri wake, Ulega.

"Inawezekana ni wakati umefika tuwe na timu ya taifa ambayo haina mahusiano na Simba na Yanga, inawezekana ikatusaidia zaidi. Tunataka kushinda na michezo ilete matokeo chanya na itoe ajira, suala la wasanii kukosa haki zao hili mkalisimamie," aliwaagiza viongozi hao aliowakabidhi kusimamia dhamana ya michezo nchini.

Katika awamu ya kwanza ya miaka mitano ya Rais Magufuli, wizara hiyo ilianza kwa kuongozwa na Nape Nnauye na kisha Dk. Harrison Mwakyembe ambaye alianguka katika mchakato wa kura za maoni kuelekea uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Katika kuhakikisha Tanzania inafanya vema kwenye mashindano mbalimbali, serikali imeahidi kushiriki kwa karibu katika maandalizi ya timu zote za taifa zinazokwenda kupeperusha bendera ya nchi.



**WENYE SOKA LAO...**



Mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo (Jezi Na. 7) na Lionel Messi wa Barcelona wakiwania kumiliki mpira katika mechi ya Kundi G ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa Uwanja wa Nou Camp juzi na Juve kushinda 3-0. Ronaldo alifunga mabao mawili kwa mkwaju wa penalti huku moja likifungwa na Weston McKennie. **HABARI UK. 20**

# FIFA KUIFUNGIA SIMBA KUSAJILI MIAKA MITATU

### ●●● Yaipiga faini ya Sh. milioni 292, bodi kujadili, lakini...

**Na Saada Akida**

WAKATI jana usiku wakitandaza 'soka biriani' [kama wanavyoliita] dhidi ya Polisi Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, mabingwa watetezi, Simba wameingia mtegoni wa kufungiwa kusajili kwa kipindi cha miaka mitatu kutokana na kukiuka taratibu za usajili, imeelezwa.

Kwa mujibu wa barua iliyoifikia Klabu ya Namungo kutoka Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), na uongozi kuthibitisha, klabu hiyo ya Ruangwa mkoani Lindi imetakiwa kutomtumia winga Shiza Kichuya iliyemsajili akiwa huru baada ya kuachana na Simba ambayo inadaiwa ilimsajili kwa kutofuata taratibu wakati bado akiwa na mkataba na klabu yake ya Pharco FC ya Misri.

Kutokana na madai hayo ya ukiukwaji wa taratibu za usajili, Simba imetakiwa kulipa dola za Marekani 127,000 sawa na takriban Sh. milioni 292.9 za Tanzania na kama ikishindwa kulipa kiasi hicho itafungiwa kufanya usajili kwa kipindi cha miaka mitatu.

Lakini, Namungo nayo imezuiwa kuendelea kumtumia mchezaji huyo hadi hapo Simba itakapolipa kiasi hicho.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari wa Namungo FC, Kindamba Namlia, juzi usiku walipokea barua kwa njia ya barua pepe [email] ikieleza mchezaji huyo hataruhusiwa kutumika kwa kuwa alisajiliwa akiwa na matatizo ya kimkataba na timu yake ya zamani ya Pharco FC na kwamba Simba inatakiwa kutekeleza taratibu hizo ndipo waanze kumtumia.

Kindamba alisema: "Sisi tulimsajili akiwa mchezaji huru hivyo bado kuna vitu ambavyo havipo sawa kwa kuwa wenye mamlaka wamesema, basi tuna kazi ya kufuatilia na kukaa chini kujua kwa sababu haya ni masuala ya sheria.

"Hatukukurupuka kufanya usajili, hivyo inabidi ujiulize kwa nini tulipata kibali cha kumtumia, kwa kuwa ni mamlaka basi tutafuata utaratibu ila tutaumia kumkosa Kichuya kwa sababu tayari alishaingia kwenye mfumo."

Hata hivyo, Bodi ya Wakurugenzi ya Simba chini ya Mwenyekiti wake, Mohammed 'Mo' Dewji inatarajiwa kukutana hivi karibuni kujadili uamuzi huo wa FIFA na hatua za kuchukua ama kukata rufani au kulipa kiasi hicho.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaimu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Mwina Kaduguda, alisema amesikia taarifa hizo lakini si rasmi kwa kuwa jana haikuwa siku ya kazi hana uhakika kama Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba (CEO), Barbara Gonzalez atakuwa ameshaipata, na kama imemfikia lazima ataitisha kikao cha bodi ili kuijadili.

"Kwa sasa sitaweza kulizungumzia suala hilo, huenda barua itakuwa imemfikia CEO wetu, ukizingatia leo si siku ya kazi nina imani kesho [leo], kama imemfikia inaweza kutufikia [bodi], ila leo [jana], tuna mechi dhidi ya Polisi Tanzania, hivyo akili yetu ipo huko," alisema Kaduguda.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >